# Nipashe

Ijumaa Januari 19, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581560

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US www.twitter.com/nipashetz www.ippmedia.com www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




**ONANA KAMILI KUITUMIKIA CAMEROON KATIKA AFCON**

UKURASA 22

## MADAI YESU ANARUDI

# Azuia wanafunzi kwenda shuleni



• **Ni** neno la kiongozi kanisani, serikali yaingilia kati... *Ukurasa 2*

**Samia** aonya CCM wenzake kashfa, njama kusaka uongozi



UKURASA 2

**RC** anadi mihogo ya Tabora kwa wanaume



UKURASA 3

**Fundi** adaiwa kujiua, aacha ujumbe kwa mjamzito wake



UKURASA 16

UKURASA WA 5

### MAJALIWA AMWAKILISHA RAIS SAMIA UGANDA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewasili Uganda akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika...

UKURASA WA 19

### MFALME, BINTI MFALME UINGEREZA WAGONJWA





MFALME wa Uingereza, Charles III, ametangazwa kuwa ana ugonjwa wa tezi dume na...

## Msajili ashtuka viongozi vyama kukosa uhalali

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Balozi Hussein Othman Katanga, anayeiwakilisha Tanzania New York, Marekani baada ya kuwasili Uganda, kumwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi na Serikali Zisizofungamana na Upande Wowote (NAM) jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**



## Uongezaji makalio rasmi Muhimbili

• **200** wawekewa puto kupunguza uzito, vitambi... *Endelea ukurasa 5*

**MICHEZO** GAMONDI AFUATA MAKALI UFUKWENI UK.24 **KATUNI** UK.6

# Awazuia watoto kwenda shuleni kwa madai Yesu karibu anarudi

**Na Elizabeth Zaya**

MWANAFUNZI Erick Manyahi aliyekuwa anasoma Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) lakini akakatisha masomo na kufungua kanisa katika Kijiji cha Chengena, Namtumbo mkoani Ruvuma, amekamatwa kwa madai ya kuwarubuni watoto 13 kutokwenda shuleni badala yake wamsubiri Yesu.

Kijana huyo anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 33, alitiwa mbaroni na Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Ngollo Malenya, baada ya kufanya msako wa nyumba kwa nyumba kutafuta wanafunzi ambao hawajaripoti shuleni. Baada ya kumbaini kijana huyo ambaye alikuwa akishirikiana na wenzake watatu, wote walihojiwa na kukiri kufanya kitendo hicho cha kuwarubuni wazazi wa watoto wasiwapeleke shuleni, bali wasome vitabu vya dini na wajiandae kumsubiri na kumpokea Yesu ambaye walidai anarudi muda si mrefu.

Licha ya watu hao kuhojiwa na mkuu huyo wa wilaya, waliendelea kuwa na msimamo wao huo.

Kijana huyo alidai kwamba alikuwa anasoma UDOM na aliamua kuacha baada ya kusoma vitabu vya dini kujua imani. Alidai kwamba anaamini elimu ya Mungu haipaswi kuchangamana na elimu ya dunia.

Ngollo akiwa ameambatana na Kamati ya Usalama ya Wilaya, aliagiza kukamatwa kwa kijana huyo pamoja na Mwinjilisti mwenzake na mke wake wanaosaidiana kwa mahojiano zaidi.

Licha ya watu hao kuhojiwa, waliendelea kusisitiza kwamba hakuna haja ya watoto kupata elimu.

"Mimi ninaishi sawasawa na kile kilichoandikwa kwamba mtu hataishi kwa mkate tu bali kwa kila neno litokalo kwa kinywa cha Mungu. Kwa hiyo kwa mujibu wa imani yangu, mimi nitakuwa mimi kwa sababu maisha si tu katika ulimwengu huu," alisema kijana huyo baada ya kuhojiwa na Mkuu wa Wilaya sababu za kuwarubuni watoto wasiende shuleni.

Alipoulizwa kama elimu yake aliyoipata tangu awali mpaka chuo kikuu haina msingi na kwa nini awarubuni watoto wao wasisome, kijana huyo alisema: "Hapana (Elimu) ni ya msingi kwa sababu kwanza mimi mpaka ninafika chuo kikuu nilikuwa katika mikono ya wazazi lakini sasa ninajitambua na mimi nina uhuru wa kuchagua kile ambacho kitanipatia furaha maishani.

"Kuwa na furaha maishani ni kutembea pamoja na Mungu. Siwezi kusema nilipoteza muda lakini kwa hili suala kujibu kwa mtu ambaye haamini, imani kwa Waadventisti Wasabato mtu anaweza asielewe vizuri lakini aliyeko ndani ya imani anaweza kuelewa."


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O.Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI YA UDALALI INATARAJIA KUUZA KUPITIA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | MAELEZO KUHUSU DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | UPENDO GODWIN LEMA | GARI | T683 DCS- NISSAN DUALIS | JODAC PROFESSIONAL CO. LTD | 30/12/2023 |
| 2 | ELIUD BAHENGAZI BALIGE | GARI | T488 DTW - TOYOTA VOLTZ | JODAC PROFESSIONAL CO. LTD | 30/12/2023 |
| 3 | BEATRIX WAKYO IKANDA | GARI | T 578 DTK -NISSAN X-TRAIL | JODAC PROFESSIONAL CO. LTD | 30/12/2023 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kubadili umiliki zitakuwa juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.




Asia Msangi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam (kushoto), akitoa maelezo kwa viongozi wa mashirika mbalimbali ya kiraia kuhusu kituo hicho kinavyoendesha shughuli za ujasiriamali wa kilimo cha mboga, walipofika kituoni hapo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**TAARIFA KWA UMMA**

**UTOAJI WA HUDUMA ZA MAWASILIANO BILA LESENI**

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuutaarifu Umma kuwa utoaji wa huduma za mawasiliano, zikiwemo huduma za usalama mtandaoni (cybersecurity services), intaneti, na vituo vya kutunzia data (data centres), katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na leseni iliyotolewa na TCRA ni kinyume na Kifungu cha 14 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 (EPOCA) ambacho kinakataza mtu, taasisi au kampuni yoyote kutoa huduma hizo bila kuwa na leseni.

Aidha, tunapenda kuukumbusha Umma kuepuka kutumia huduma za mawasiliano, zikiwemo huduma za usalama mtandaoni, intaneti, na vituo vya kutunzia data, zinazotolewa na mtu, taasisi au kampuni zisizo na leseni zilizotolewa na TCRA.

TCRA inaendelea kusimamia huduma za mawasiliano nchini na haitasita kuchukua hatua kisheria dhidi ya mtu, taasisi au kampuni itakayobainika kujihusisha na utoaji wa huduma za mawasiliano, zikiwemo huduma za usalama mtandaoni, intaneti na vituo vya kutunzia data, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na leseni iliyotolewa na TCRA

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia nambari 0800 008 272 au baruapepe: dawatilahuduma@tcra.go.tz .

Imetolewa tarehe **18 Januari 2024.**

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz


# Samia awaonya CCM wenzake katika njama za kusaka uongozi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, ameonya wana CCM wanaohujumiana katika mchakato wa kutafuta uongozi uchaguzi mkuu.

Alitoa onyo hilo wakati akikamilisha ziara yake ya mikoa minne ya kichama wakati akifungua tawi la CCM Tasani Jimbo la Makunduchi, Mkoa wa Kusini Unguja.

"Mwakani tunaingia kwenye kazi ile... kazi yetu kubwa najua wengi mtavutika kuingia kwenye kazi tofauti ombi langu kwenu msihujumiane, wazuri wachapa kazi wapewe nafasi," alisema.

Alisema sio vibaya kupanga safu, lakini ni vyema kuipanga itakayovusha Chama Cha Mapinduzi na sio itakayomvusha mtu na kwenye chaguzi zinazokuja.

"Lakini kubwa ni kutokuhujumiana mwenye uwezo apewe nafasi tupange safu ili mwaka 2025 chama chetu kiende vizuri," alisema Dk. Samia.

Akizungumzia ujenzi wa tawi la Tasani, alisema kuwa na tawi zuri ni jambo moja, lakini uwanachama na uimara wa CCM ni wanachama wenyewe kuwa na umoja na kujitambua.

"CCM imara sio tawi, tawi linaweza kufungwa na likawa halina kazi, uanachama imara, chama imara ni vikao ni kazi zetu zifanyike ndani ya tawi," alisisitiza.

Alisema amegharamika kutoa Sh. milioni 76 kwa ajili ya ukarabati wa ujenzi wa tawi hilo na fenicha na kumwagiza mbunge na Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi kununua vitendea kazi kwa ajili ya matumizi ya chama katika tawi hilo.

Rais Samia aliupongeza uongozi wa mkoa huo kwa kufanikisha vizuri uandikishaji katika daftari la wapigakura wapya na kuutaka uongozi huo kuwashawishi wapenzi wa CCM hasa vijana kuendelea kujiunga na chama na kukipigia kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Alisema uhai wa chama ni wanachama hivyo lazima viongozi wajitahidi kuwashawishi vijana kujiunga na chama ili kuongeza nguvu na kiendelee kubaki kuwa imara.

Akisoma risala ya tawi la Tasani, Abeid Mtwana Haji, alisema ujenzi wa tawi hilo umegharimu Sh. milioni 55 na wanachama wa tawi hilo ifikapo uchaguzi wa 2025 watajitokeza kwa wingi na kukiletea ushindi kwenye uchaguzi huo.

Alisema uongozi wa tawi kwa kushirikiana na shehia wameshirikiana kuwakusanya na kuwahamasisha vijana kujiandikisha katika daftari la wapigakura na wamefanikiwa kwa asilimia 98.

Katika hatua nyingine, Dk. Samia ameongoza mkutano na Halmashauri za CCM za wilaya zote za Unguja na kamati za siasa za wilaya na mikoa, Mkoa wa Kusini Unguja.

HABARI KITAIFA

# RC anadi mihogo ya Tabora kwa wanaume

**Na Halfani Chusi**

MKUU wa Mkoa Tabora, Balozi Dk. Batilda Buriani (pichani), amesema utafiti uliofanywa na wataalamu, umebaini mihogo aina ya TARI Tumbi IV inaongeza nguvu za kiume.

Balozi Dk. Batilda aliyasema hayo jana mkoani mwake alipotoa taarifa hiyo kwa vyombo vya habari, akiwataka kinamama kutumia chakula hicho kulinda ndoa zao.

Alisema mikoa yote, ukiwamo wa Dar es Salaam, itambue kwamba utafiti huo umebaini mihogo hiyo ya aina yake, yenye kiwango kikubwa cha zinki, inasaidia kutatua tatizo la upungufu wa nguvu za kiume.

"Wenzetu kwa mfano kule Dar es Salaam wanatumia mihogo, nazi na karanga kwa ajili ya 'kubusti', lakini uzuri kwa sasa tuna hii mihogo yenye zinki nyingi," alisema.

Tatizo la upungufu wa nguvu za kiume linatajwa kuwa janga nchini. Rais Samia Suluhu Hassan katika moja ya hotuba zake, Oktoba 2022 aliagiza wataalamu kufanya utafiti kuhusu tatizo hilo.

"Kuna shida kwa hawa vijana wetu na mnaijua na mnaficha, fanyeni utafiti na kwa sababu ni jambo la siri, halisemwi,



linaumiza zaidi vijana wetu.

"Mara sijui vumbi la kongo, mara mchuzi wa pweza, lakini tatizo kubwa lipo kwenye lishe. Tatizo letu liko kwenye lishe. Tatizo liko wapi? Kwenye lishe. Sasa watafiti tafuteni tunafanyaje watoto wetu wawe shababi, waweze kuzaa watoto wenye afya. Jamii hii ni yetu sote," Rais Samia aliagiza.

# Msajili ashtuka viongozi wa vyama kukosa uhalali

**Na Elizabeth Zaya**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa imesema kuna idadi kubwa ya vyama vya siasa ambavyo muda wa viongozi wake unaisha na kuvitaka kufanya uchaguzi.

Ofisi hiyo ambayo ndio yenye jukumu la kulea vyama hivyo, imesema kifungu cha 9(2)(e) kikisomwa pamoja na kifungu cha 8D (1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa Sura ya 258, kinaelekeza kila chama cha siasa kufanya uchaguzi wa kidemokrasia wa viongozi wake kwa vipindi ambavyo vimewekwa katika katiba yake.

Kwa mujibu wa maelezo ya barua iliyoandikwa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kwenda kwa vyama hivyo, kanuni ya 16 ya kanuni ya vyama vya siasa inaelekeza uchaguzi wa viongozi wa chama cha siasa unapaswa kufanyika si zaidi ya miaka mitano tangu uchaguzi uliopita.

Pia inaelekeza chama kitaomba rukhsa ya Msajili wa Vyama vya Siasa endapo kinataka kufanya uchaguzi zaidi ya kipindi hicho.

"Hivyo, vyama vya siasa ambavyo muda wa uongozi wa viongozi wake unakaribia kuisha, vinakumbushwa kufanya uchaguzi wa viongozi wake kabla ya muda huo kuisha," inaelekezwa kupitia barua hiyo ya Ofisi ya Msajili kwa vyama hivyo.

**WENYEWE WALONGA**

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia maelekezo hayo ya Msajili, alikiri kuona barua hiyo. Uongozi wa chama chao bado ni halali.

"Tumeiona hiyo barua ya Msajili na ambayo ofisi yake imeisambaza kwenye mitandao ya kijamii. Kwa upande wetu (CHADEMA), uongozi wetu ni halali mpaka mwishoni mwa mwezi Desemba, 2024, hivyo Msajili anavikumbusha vyama ambavyo si sisi CHADEMA.

"Ila tulishaanza uchaguzi ngazi za chini na tunaendelea katika ngazi mbalimbali nchini kwa mujibu wa ratiba yetu," alisema.

Mkurugenzi wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma wa Chama cha Wananchi (CUF), Mohamed Ngulangwa, alisema kwa sasa wanafanya uchaguzi wa ndani na wanatarajia kufanya mkutano mkuu wa kitaifa kabla ya mwezi Septemba, mwaka huu, ili kukidhi matakwa ya Katiba ya chama.

"Kwa mujibu wa Katiba yetu, kiongozi yeyote anaweza kugombea na kuchaguliwa tena mradi tu wapigakura bado wana imani naye, muda wa uongozi unapokamilika na uchaguzi kufanyika, watakaochaguliwa ndio chaguo la Katiba ya chama," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema kwa sasa wao wanaendelea na uchaguzi na wako ngazi ya mikoa.


# TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED**, kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za mdaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya Siku Tatu (3) kama rudio la tangazo kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ABDALLAH HASSANI JUMA | ABDALLAH HASSANI JUMA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK045156, ARDHI NA.TMK/CHB/RTT35/300A | RANGI TATU, CHARAMBE MANISPAA YA TEMEKE | 22/01/2024, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |
| 2 | ABDALLAH HASSANI JUMA | ABDALLAH HASSANI JUMA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.TMK045157, ARDHI NA.TMK/CHB/RTT35/300 | RANGI TATU, CHARAMBE MANISPAA YA TEMEKE | 22/01/2024, SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED**
**P.O.BOX 1305**
**Songea, Ruvuma**
**Tel: 0757 940 064/ 0716 070 298 / 0784 718 734**
**Email: twinscoltd5@gmail.com**




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza wakati wa mjadala wa 'kutengeneza fursa katika ardhi ya Afrika' uliofanyika katika Mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani (WEF) Davos, Uswisi jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# TRC yasitisha safari za treni mikoa 12 kupisha ukarabati

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limesitisha kwa muda huduma za safari za treni katika mikoa 12 ili kupisha ukarabati wa miundombinu baada ya kuathiriwa na mvua inayoendelea kunyesha.

Kwa reli ya kati, safari zake zinatarajiwa kurejeshwa Januari 23, mwaka huu na kwa mikoa ya kaskazini; Tanga, Kilimanjaro na Arusha, zitarejeshwa kuanzia Januari 29, mwaka huu baada ya kukamilika uimarishaji miundombinu.

Kwa mujibu wa taarifa ya TRC iliyotolewa jana, safari zilizositishwa zinaigusa mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Singida, Tabora, Katavi na Kigoma. Pia Shinyanga, Mwanza, Tanga, Kilimanjaro na Arusha.

Maeneo yaliyobainishwa kuwa na uharibifu huo ni: Mazimbu, Kilosa na Munisigara, mkoani Morogoro; Godegode na Gulwe mkoani Dodoma; Ruvu Junction, Wami na Mvave, mkoani Pwani pamoja na eneo la Mkalamo, mkoani Tanga.

"Wahandisi kutoka TRC wanaendelea na matengenezo katika maeneo yaliyoathirika na mvua inayoendelea kunyesha. TRC inaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza na inawasihi wananchi kuwa wavumilivu katika kipindi cha matengenezo, ili kuhakikisha usafiri unarejea katika hali ya usalama," shirika hilo lilibainisha katika taarifa yake hiyo.

Mara kadhaa hususani kipindi cha mvua, miundombinu ya reli imekuwa inaharibika na kusababisha usumbufu wa abiria wanaotumia usafiri huo.

Januari 12, mwaka huu, abiria zaidi 1,200 waliokuwa wanasafiri kwa treni kutoka Dar es Salaam kuelekea Kigoma, walikwama katika kituo cha Morogoro baada ya kipande cha kutoka mkoani humo kuelekea Dodoma kuathiriwa na mvua.

Katika kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Usalama wa Reli mwezi Oktoba, mwaka jana, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Uchukuzi, Dk. Ally Possi, aliiagiza TRC kuboresha miundombinu ya reli iliyoharibika ili kuhakikisha usalama na usafiri bora kwa wananchi.

# Biteko: Serikali imedhamiria kuwekeza miradi ya umeme

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema serikali imeamua kwa dhati kuwekeza katika miradi ya nishati ili kuhakikisha upatikanaji umeme unakuwa mkubwa kuliko mahitaji ya nchi.

Dk. Biteko alisema jana jijini Dodoma wakati Wizara ya Nishati ilipowasilisha taarifa kuhusu hali ya uzalishaji na usambazaji umeme mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, Katibu Mkuu, Mhandisi Felchesmi Mramba, baadhi ya wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara na watendaji wa wizara.

" Moja ya vipaumbele vikubwa vya serikali ni sekta ya nishati na ndiyo maana fedha zimekuwa zikitolewa za kutekeleza miradi mbalimbali ya ukiwamo mradi mkubwa wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao gharama yake ni Sh. trilioni 6.5 mpaka sasa serikali imeshamlipa mkandarasi Sh. trilioni 5.7 sawa na asilimia 88.7," alisema.

Kuhusu usimamizi wa mradi wa JNHPP, alisema serikali iko makini katika usimamizi na kwamba kuna mamlaka mbalimbali zinazosimamia mradi huo ili ukamilike kwa wakati na kwa ufanisi. Alitoa mfano wa miongoni mwa wasimamizi Timu Maalumu ya Wataalam iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kusimamia mradi huo, inayoongozwa na Prof. Idris Kikula.

Kuhusu hali ya miundombinu ya umeme nchini, Biteko alisema itaendelea kufanyiwa matengenezo ili kuzalisha, kusafirisha na kusambaza umeme kwa ukamilifu wake, huku juhudi za kujenga miundombinu mingine upya zikiendelea.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Gissima Nyamo-Hanga, aliielekeza kamati hiyo kuwa mradi wa JNHPP kwa sasa umefikia asilimia 95.8 na kwamba mtambo namba tisa utakaozalisha megawati 235 umeshakamilika na mtambo namba nane na namba saba iko mbioni kukamilika.

Kuhusu hali ya umeme nchini, Mhandisi Nyamo-Hanga alisema pamoja na jitihada mbalimbali zinazoedelea kufanywa na serikali ili kupunguza tatizo la nishati hiyo, hali ya upungufu wa umeme itaisha baada ya kuwashwa kwa mashine mbili za JNHPP zenye uwezo wa kuzalisha megawati 470 kabla ya Machi, mwaka huu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dk. David Mathayo, kwa niaba ya wajumbe, alipongeza viongozi wa Wizara ya Nishati kwa usimamizi mzuri wa sekta na kueleza kuwa wana imani viongozi hao kwa kushirikiana na taasisi zake wataiwezesha nchi kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika.

# Wananchi 515 waondoka Ngorongoro kwa hiari

**Na Jenifer Gilla**

KAYA 72 zenye wananchi 515 na mifugo 2,206 zilizokuwa na makazi katika Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA), jana ziliondoka katika eneo hilo kuelekea Kijiji cha Msomera, Halmashauri ya Handeni, mkoani Tanga.

Kaya hizo ni miongoni mwa 525 zilizojiandikisha kuhama kwa hiari katika awamu ya pili ya mradi huo wa kuhama hifadhini kwa hiari. Kaya 126 tayari zimeshahama na zilizobaki serikali inaendelea na utaratibu wa kuhamisha.

Kamishna wa Uhifadhi NCAA, Richard Kiiza, alisema kundi la awamu hiyo ndio kubwa zaidi kuondoka tangu kuanza utekelezaji mchakato huyo mwaka jana.

Alisema kadri ujenzi wa nyumba za makazi unavyoendelea katika vijiji vya Msomera, Kitwai na Saunyi, idadi ya wananchi wanaojiandikisha kuhama kwa hiari imeendelea kuongezeka. Hadi sasa, zaidi ya kaya 1,070 zimeshajiandikisha.

Kamishna Kiiza alisema ujenzi wa nyumba 5,000 katika vijiji hivyo unaendeela chini ya SUMA JKT na tayari zaidi ya nyumba 360 zimeshakamilika na nyumba zingine zaidi ya 2,000 ziko katika hatua mbalimbali za ujenzi.

Aliwahimiza wananchi walioagwa jana kuendelea kuwa mabalozi wa kuwahimiza waliobaki kujiandikisha kuhama kwa hiari ili wanufaike na maisha bora yaliyoandaliwa na serikali nje ya hifadhi.

Meneja wa Mradi wa Kuhamisha Wananchi Wanaoishi Ndani ya Hifadhi hiyo, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Fedes Mdala, alisema kundi hilo litafikisha idadi ya kaya 749 zenye watu 4,337 na mifugo 19,915 zilizohama hifadhini.

Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro, Kanali Wilson Sakulo, alisema kuwa wananchi hao wamepewa stahiki zao zote za msingi ikiwamo nyumba yenye hati kwenye eneo la ukubwa wa ekari 2.5 na shamba kwa ajili ya kilimo lenye ukubwa wa ekari tano.

Alisema katika kijiji wanachokwenda, kuna huduma zote muhimu kama vile maji, shule, kituo cha kutolea huduma za afya, barabara, mabwawa, majosho, minada, umeme na mawasiliano na kupata uhuru wa kufanya shughuli za kilimo na kuishi maisha huru tofauti na hifadhini.

Kanali Sakulo alielekeza uongozi wa NCAA kuendelea kutoa elimu, uhamasishaji na uandikishaji wananchi walio tayari kuhama kwa hiari na kuhakikisha kila aliyejiandikisha kuhama, anahamishwa kwa wakati na kupata stahiki zake zote.

Pia alielekeza kuhakikisha wananchi wanaohama hawarudi tena katika maeneo hayo kwa kuwa serikali imeshawajengea mazingira wezeshi yenye huduma zote muhimu za kijamii.

Mmoja ya wananchi waliohama jana, Petro Tengesi, alishukuru serikali kwa upendo wake kwa wananchi wa Ngorongoro na kuendelea kuwajengea mazingira bora nje ya hifadhi na kuwalipa stahiki zao kwa wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mobhare Matinyi, alisema lengo la serikali ni kuwajengea maisha bora wananchi hao kwa kuwapeleka eneo ambalo watakuwa huru kufanya shughuli za maendeleo ambazo haziruhusiwi ndani ya hifadhi kwa mujibu wa sheria.



Naibu Mkurugenzi wa Halotel Sekta ya Biashara, Bui Van Thang, akiwa pamoja na mshindi wa gari wa kampeni ya Kivumbi na Halotel aina ya MAZDA CX5, Kassim Seif Mbufu (katikati), wakati wa makabidhiano jana katika duka la Halotel Palm Village Mikocheni, Dar es Salaam. Habari UK. 8. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MNH kuanza huduma uongezaji makalio, matiti Juni

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Profesa Mohamed Janabi, amesema watu 200 wamewekewa maputo kwa ajili ya kupunguza unene na kuokoa Dola za Kimarekani milioni tatu (sawa Sh. bilioni 7.54).

Kadhalika, MNH imesema kabla ya mwezi Juni, mwaka huu inatarajia kuanza kutoa huduma ya kuongeza makalio na matiti na pia kuyapunguza.

Taarifa iliyotolewa jana jijini Dar es Salaam kwa vyombo vya habari, ilisema tangazo rasmi la MNH lilikuwa la puto na kupunguza wenye uzito mkubwa wa kilo 90 kwenda juu.

"Wanufaika wa kupunguza uzito kwa njia hii waliofanyiwa wako salama ni karibu 200. Ina maana gani hawa Watanzania wangeenda Uturuki ama Afrika Kusini (SA), inakadiriwa ni Dola za Kimarekani 15,000 ukizidisha mara 200 ni Dola za Kimarekani 3,000,000," alisema Janabi na kuongeza;

"Fedha hizo zimeokolewa kwenda nje ya nchi. Madaktari wetu wanapata ujuzi maana tumefanya pamoja na Profesa mbobezi kutoka India."

Aidha, Janabi alitoa ufafanuzi wa MNH kuanza kutoa huduma za kuongeza makalio, kuongeza matiti na kupunguza kabla ya Juni, mwaka huu.

Alisema ukweli kutoka MNH kuhusu taarifa ya kuongeza makalio ni upasuaji maarufu duniani, sio dharura ni uamuzi wa mtu binafsi kuwa haridhiki na mwonekano alionao na kuchagua anachokitaka.

Janabi alisema upasuaji huo hauhitaji mtambo maalum ni ultrasound mashine inakupa mwongozo sindano yako inapokwenda.

"Madhara (maumivu pale sindano itakapopigwa) na kidonda kidogo pale palipochanwa sentimita kati ya 2-3. Jina lake la kitaalamu ni Brazilian Butt Lift," alisema Janabi.

Pia alisema kuwa Muhimbili haijawahi kutoa tangazo la marekebisho ya makalio.

"MNH ni hospitali bobezi ni muhimu kufanya procedures (upasuaji) tofauti na hospitali ndogo. Faida tutapunguza fedha chache za kigeni kwenda nje, tutawapa nafasi wataalamu kwenda na vitu walivyojifunza na kuleta wageni kutoka nje (Medical Tourism)," alisema.

# Majaliwa amwakilisha Rais Samia Uganda

**Na Mwandishi Wetu,** KAMPALA



WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani), amewasili Uganda akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika Mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi na Serikali zisizofungamana na upande wowote (NAM) ulioanza Januari 15, mwaka huu.

Majaliwa aliyetua Uganda jana, pia atamwakilisha Rais Samia katika mkutano wa Tatu wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Kundi la G77+China utakaofanyika tarehe 21-22 Januari, mwaka huu jijini Kampala. Mkutano huo unaotarajiwa kushirikisha nchi wanachama wapatao 134.

Ujumbe wa Waziri Mkuu katika mikutano hiyo utajumuisha viongozi waandamizi wa serikali akiwamo Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba.

Mkutano wa NAM hufanyika kila baada ya miaka mitatu na mkutano wa mwisho wa 18 ulifanyika jijini Baku, Azerbaljan mwezi Oktoba, 2019. NAM ni umoja wa nchi na serikali 120 zenye msimamo wa sera ya kutofungamana na upande wowote.

Umoja huo ulianzishwa wakati wa enzi za vita baridi ili kusaidia nchi wanachama wake kutoka mabara ya Asia, Afrika na Latin Amerika kuondokana na ukoloni ili kujitawala kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, January, alisema jana kuwa katika mkutano huo kutakuwa na ajenda muhimu zitakazojadiliwa na kuamuliwa na wakuu wa nchi.

"Katika mkutano NAM kutakuwa na maazimio mahususi yanayohusu masuala ya maendeleo ya uchumi, kijamii, ajira, ushirikiano wa kikanda na kimataifa, amani na usalama na masuala mengine yanayohusu nchi hizi zisizofungamana na upande wowote," alisema.

Mkutano huo unalenga kuimarisha ushirikiano kwenye masuala ya biashara, uwekezaji, kutokomeza umaskini, mabadiliko ya tabianchi, amani na usalama katika mipaka, sekta ya afya, mandeleo endelevu, na uchumi wa kidijiti.

Rais wa Uganda, Yoweri Museveni ndiye mwenyekiti wa mkutano huo na anatarajiwa kukabidhiwa rasmi Uenyekiti wa Kundi hilo kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Cuba, Miguel Mario Diaz-Canel Bermúdez.


NSSF
Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**TAARIFA KWA UMMA**

**ZOEZI LA UHAKIKI WA WASTAAFU NA WATEGEMEZI**

**Januari 19,2024**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) unawatangazia wastaafu na wategemezi wote wanaolipwa pensheni kila mwezi kuwa, kutakuwa na zoezi la uhakiki litakaloanza tarehe **1 Februari, 2024** hadi **30 Aprili, 2024.** Zoezi hili litafanyika Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi saa 10:30 jioni kwenye ofisi zote za NSSF za mikoa yote. Kwa wastaafu waliopo Unguja na Pemba, uhakiki wao utafanyika ofisi za ZSSF. Aidha kwa wastaafu waliopo Dar es Salaam, uhakiki wao utafanyika katika ofisi za mikoa ambazo ni **ILALA, TEMEKE, KINONDONI, UBUNGO, MBEZI BEACH na KIGAMBONI**

Mstaafu anatakiwa kufika na nyaraka zifuatazo:

- Kitambulisho cha NSSF au kuponi ya pensheni,
- Kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA,
- Picha moja ndogo ya sasa ya rangi (passport size) kwa wale ambao hawakufanya uhakiki kwa mwaka 2023,
- Kwa wategemezi (watoto) tafadhali fika na cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha shule
- Kwa wastaafu wagonjwa au wazee wasiojiweza, taarifa itolewe kupitia barua pepe **customercare@nssf.go.tz** au piga simu ya bure **0800116773** au taarifa ziwasilishwe kwenye ofisi ya NSSF iliyo karibu

**ANGALIZO:** Malipo ya pensheni ya mwezi **JUNI 2024** yatafanyika kwa wastaafu na wategemezi ambao wamehakiki tu

**ATAKAYESIKIA TANGAZO HILI AMTAARIFU NA MWENZAKE**

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu kuhusu kujiandaa kustaafu itiliwe mkazo

**KUNA** msemo kwamba unapoanza kazi unaanza kujiandaa kustaafu. Ni msemo uliozoeleka katika jamii kusisitiza umuhimu wa mtu kufanya maandalizi ya maisha baada ya ajira au utumishi.

Pamoja na msemo huo kuwamo miaka na miaka, ni wachache wanaozingatia na kujiandaa huku wengine wakijipambanua kwamba ni wastaafu. Watu hao huanza kujiwekea akiba na kuandaa mazingira ya kuondoka kwenye ajira hata kabla ya muda wa kustaafu kuwadia. Katika watu hao, wako wale ambao hutumia ajira kama sehemu ya kujipatia mtaji kwa ajili ya kuanzisha shughuli za ujasiriamali ili kujipatia kipato nje ya ajira.

Wakati kundi hilo likifanya hayo kwa maandalizi ya maisha nje ya ajira, wengi huendelea kufanya kazi na kufanya mambo kwa mazoea. Hawana muda wala mawazo ya kijiandaa kustaafu na tegemeo lao kubwa ni mafao ya kustaafu. Wako wengine ambao hata baada ya muda wa kustaafu kufika huomba kuongezewa muda ili kuendelea kufanya kazi.

Matokeo ya kustaafu bila kujiandaa yamewafanya wengi kuingia katika matatizo makubwa na majuto. Hali hiyo hutokana na kutumia mafao ya kustaafu kujenga nyumba au kuanzisha biashara wasizo na uzoefu nazo.

Wako ambao wameingia kwenye mtego wa mabasi kwa ajili ya kusafirishia abiria ndani ya miji mikubwa ama kwa kushawishiwa au kudanganwa kuwa ni biashara inayoingiza fedha haraka na kuleta matunda chanya ya uwekezaji. Baada ya muda mfupi, wanaambulia kujuta kwa kupoteza fedha kwa kuingiza kwenye biashara ya hasara.

Matokeo ya kupoteza fedha kwa kufanya biashara hizo ambazo zimesababisha matatizo kwao, baadhi wamepata maradhi kama vile ugonjwa wa moyo, kisukari, kiharusi na msongo wa mawazo. Kutokana na kukumbwa na maradhi hayo, baadhi wamepoteza maisha muda mfupi baada ya kustaafu, hivyo kutokufaidi matunda ya utumishi wao serikalini au sekta binafsi.

Kutokana na kuwapo kwa athari hizo, baadhi ya taasisi zimechukua jukumu la kuwaandalia semina waajiriwa wao ambao wanakaribia kustaafu ili kupata elimu ya namna ya kuishi nje ya ajira. Kuwapo kwa semina hizo kumesaidia kwa kiasi fulani kwa watu kuishi bila kuwa na msongo wa mawazo na kupata maradhi hatari kwa maisha yao.


Mwendelezo wa semina na mafunzo hayo, ulifanywa wiki hii na Wizara ya Fedha kuhusu elimu ya fedha iliyofanyika mjini Morogoro na katika moja ya mada, ilisisitizwa watu kujenga utamaduni wa kujiwekea akiba kwa matumizi baada ya ukomo wa ajira. Pia imesisitizwa kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii ili wanapostaafu wasiwe mzigo wa utegemezi kwa familia au ndugu na jamaa.

Ni wazi kwamba mtu anahitaji fedha kwa ajili ya masuala ya msingi awapo kazini au nje ya kazi, hivyo maandalizi kwa ajili ya kustaafu hasa kujiwekea akiba ni jambo la muhimu. Kwa mantiki hiyo, elimu kuhusu maisha baada ya utumishi au ajira yana umuhimu wa kipekee ili kumwandaa mtu kuishi maisha mazuri baada ya umri wa kustaafu kufika.

Pamoja na ukweli huo, ni vyema mafunzo hayo yakaboreshwa kwa kuyaendesha kwa mfumo wa rika badala ya miaka miwili au mitatu kabla ya kustaafu. Waajiri au taasisi zilizobobea katika ushauri elekezi na mafunzo wanapaswa kufanya mafunzo hayo ama miaka 20 au 10 hata mitano ili kumwandaa mtu kujiweka sawa kwa maisha baada ya ajira.

Kwa kufanya hivyo ni dhahiri kwamba wafanyakazi wakiwa bado wana nguvu watapata mafunzo ambayo yatawasaidia kujiweka katika hali nzuri na kuhimili mikikimikiki ya kustaafu na kuepuka msongo wa mawazo au kutapeliwa na hatimaye kukumbwa na kiharusi na maradhi ambayo yatasababisha kupoteza maisha mapema.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tunapofuata taratibu, vita vizito kukabili TB vinageuka kuwa nafuu

Na Tuntule Swebe

**UGONJWA** kifua kikuu ambao wenyewe kwa lugha ya kizungu au kitaalamu wanauita 'tuberculosis' si mgeni, ila madhara yake yanaifanya iwe ngeni kwetu. Kwa kifupi imezoeleka TB.

Ni maradhi yanayoambukiza kwa njia ya hewa, iwe mtu anapokohoa au kupiga chafya, hata mate ya mgonjwa yakiwa hewani kwa kiasi kikubwa.

Ugonjwa huo ni hatari na chanzo cha vifo vingi. Inaanza penye bakteria mbalimbali kusambaa hususan mapafu, nayo yana kawaida ya kuathirika, hata inaangukia madhara makubwa.

Mtu anaishia kuwa madhara makubwa. Je, nini kifanyike? Kwanza tuamini, mtu yeyote anaweza kuupata ugonjwa huo. Kwa kiasi kikubwa, unawapata hasa watu wanaosumbuliwa na upungufu wa kinga, kama wenye Virusi vya Ukimwi.

Bakteria hao wanapoingia mwilini, ni vigumu sana kugundua na dalili zake hazionekani mara moja, hadi pale unapokuwa ugonjwa kamili.

Binadamu inakupasa uzingatie kanuni za afya, ndipo unapoweza kugundua hayo. Unastahili kufanya nini, unapomhudumia mgonjwa wa TB?

Mgonjwa anashauriwa kuziba mdomo pindi anapokohoa au kupiga chafya, ni hali inayosaidia kuepusha maambukizi.

Mgonjwa anatakiwa pia kumaliza dozi aliyoandikiwa na mganga wa kituo cha afya, ili kuepusha ugonjwa huo kurejea katika afya yake, baada ya kujificha. Hivyo ni hatari kwa mgonjwa kukatisha dozi

Mgonjwa anapomaliza dozi, anatakiwa kuangalia tena afya yake kama amepona au la? Hivyo, akifuata maelekezo anaweza kupona kabisa pasipo shaka.

Dalili kamili za ugonjwa huo, ni mtu kuwa na kikohozi cha kupitiliza tena kinachouma wiki mbili mfululizo au tatu na wakati mwingine, mgonjwa wa kifua kikuu anatokwa na jasho jingi

Pia, kuna wakati mwingine mgonjwa anavimba sehemu za mwili kama vile kwapani, akijihisi ni mdhaifu, huku akipungua uzito wa mwili .

Hivyo, mtu anapokuwa katika dalili hizo ni muhimu kuwaishwa kwenye kituo cha afya kwa ajili ya vipimo na matibabu.

Nao watoto ili kuepushwa na maambukizi ya kifua kikuu kikali, wanapaswa kupewa chanjo kama kinga dhidi ya ugonjwa huo,

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, watu 79 hufa kila siku kwa ugonjwa wa kifua kikuu. Hapo nakumbuka mnamo Julai, mwaka jana, Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, alitaja takwimu za dunia zina onyesha watu takribani million 10.5 wanaambukizwa kifua kikuu kila mwaka.

Pia, siku ya Machi 24 mwaka jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa naye akawataka wananchi waungane na serikali, pia na wadau wa maendeleo katika vita kukitokomeza ugonjwa kifua kikuu.

Inaelezwa kwamba kwa watoto, kifua kikuu kimekuwa kikilinganishwa na magonjwa mengine, watoto katika mtihani wa kujieleza na hata inakuwa vigumu kujua kama wameambukizwa.

Kwa mujibu wa asasi moja isiyo ya kiserikali, ni kwamba ugonjwa unawaandama zaidi watu wenye maradhi ya Ukimwi, kutokana na kinga zao kuwa chini.

Hapo inakuwa muhimu kitaifa, umma kwa pamoja kupambana na ugonjwa huo, kifua kikuu, kwani ni hatari na chanzo cha vifo vya watu wengi.

Hivyo, pindi mtu anapohisi hali ya udhaifu usioeleweka mwilini, anapaswa afike haraka kwenye kituo cha afya kupatiwa matibabu.

Anapotajwa mwenye maambukizi ya VVU, anashauriwa kwenda kwenye kituo cha afya ili kuangalia zaidi afya yake na kuanza kutumia dawa mapema hiyo, itasaidia kuepuka maradhi kama kifua kikuu, mwili na afya itabaki salama. Mtu ataweza kuishi ndani ya msukosuko hiyo ya maradhi na kimazingira.

Kwa ujumla, mwenye kifua kikuu naye ana haki ya kupata huduma stahiki kwa mujibu wa miongozo, sheria na kanuni za afya.

Mara zote mtu anapogundulika kuumwa, huanza kwa kupewa dawa na umakini wa kiafya hatua zinaanza kuchukua nafasi.

Mtu huyo katika siku za mwanzo, anapokohoa ana kuwa hatari kuambukiza, lakini akishaanza dozi, anabaki salama kwa wote hawaambukizwi, nguvu ya dawa inafanya kazi yake.

Kwa mujibu wa kanuni za afya na hata ustaarabu wa kijamii, mtu anapokohoa anatakiwa kuuziba

HABARI KITAIFA



Sehemu ya daraja lililokatika Mazinge, Kata ya Ndembezi, Manispaa ya Shinyanga, ambapo wananchi wameiomba serikali kuwajengea haraka ili kurudisha mawasiliano ya barabara kutokana na mvua inayoendelea kunyesha hapa nchini Habari Uk. 10. **PICHA: MARCO MADUHU**

# ACT yasema hakuna kukata tamaa kuleta mageuzi nchini

**Na Mwandishi Wetu,** TANDAHIMBA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka wanachama wa chama hicho na wananchi kutokata tamaa na kujenga imani kwa kuwa mageuzi nchini Tanzania ni jambo linalowezekana.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo Wilaya ya Tandahimba katika Kijiji cha Ndimba, mkoani Mtwara alipozungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara wa chama hicho akiwa katika ziara maalumu ya kichama.

Alisema, suala la mageuzi ni jambo la kudai haki na kwamba sio rahisi iwapo wananchi hawataonesha jitihada ya kushirikiana kwa pamoja kupigania mageuzi ya kiuchumi na kimaendeleo ndani ya nchi yao.

Alisema ushirikiano na kuwapo uongozi thabiti uliochaguliwa na wananchi wenyewe utawawezesha kuwatetea na kupigania haki za wanyonge ikiwamo kuleta mabadiliko katika bei za mauzo ya mazao ikiwamo korosho zinazozalishwa kwa wingi na wananchi wa mkoa huo wa Mtwara.

Alisema bei ya mazao ya wakulima kama korosho ilivyo sasa ni unyonyaji na haimfaidishi mkulima jambo linalowavunja moyo na njia pekee ya kuondoa tatizo hilo ni wananchi kuungana kupigania kuwapo mageuzi ya kweli ya uongozi nchini Tanzania.

Alisema bei ndogo ya ununuzi wa mazao ya wakulima ni kero kubwa kwa wananchi wa mkoa wa huo hasa wakulima wa korosho na kuwataka waunge mkono chama cha ACT kwa vile kimejipambanua kutetea haki za wananchi na kupigania kuondoa kero na changamoto.

Alisema mazingira ya sasa ya kuwapo viongozi wanaoishauri serikali kwa kuzingatia maslahi yao binafsi ndio chanzo kikubwa cha kuwapo bei ndogo ya ununuzi wa mazao ya wakulima nchini ikiwamo zao hilo na wananchi wa mkoa huo wanalalamikia bei ya Sh. 1,000 ni kumnyonya mkulima.

Alisema korosho ni biashara kama zilivyo nyingine ambayo inaweza kuwanufaisha ipasavyo wakulima na kwamba ni kumdhulumu mwananchi anayefanya juhudi za kuzalisha halafu asifaidike na anachokizalisha yeye mwenyewe na badala yake jasho lake likawafaidisha watu wengine.

Alisema malalamiko ya wananchi wa Mtwara kuhusu zao hilo kupewa bei ya Sh. 1,000 ni ya msingi kwa kuwa wajanja wanauza korosho hizo baada ya kusarifu kidogo kwa bei ya Sh. 20,000 kwa nusu kilo inayomnyima haki ya jasho lake mkulima.

Hata hivyo, amewaahidi wananchi hao suala hilo pamoja na kero nyengine walizonazo atazipeleka serikalini ili kufanywe juhudi za kisera kuleta ufumbuzi ikiwamo kupatikana bei mwafaka ya mazao kama inavyofanyika nchi nyingine.

Aliwataka Watanzania kuendelea kukiunga mkono chama cha ACT kwa kuwa viongozi wake wamejipambanua kuendelea kushirikiana na wananchi kupigania mageuzi ili kuleta maendeleo ya Watanzania kiuchumi na kijamii.

Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, yupo Tanzania Bara akiwa na ziara maalum ya kichama katika mikoa ya Kusini mwa Tanzania na tayari amewasili mkoani Lindi kuendelea na ziara yake hiyo Mkoa wa Lindi kabla ya kuondoka kuelekea mkao wa Pwani.

# Serikali yathamini miradi maendeleo kutoka kwa wadau

**Na Steven William,** MKINGA

MKUU wa Wilaya ya Mkinga, Kanali Maulidi Surumbu, amesema miradi inayotekelezwa na wadau wa maendeleo likiwano Shirika la World Vision Tanzania, imesaidia kuwahudumia wananchi kimaendeleo.

Kauli hiyo aliitoa juzi kwenye hafla ya kukabidhiwa miradi miwili yenye thamani ya Sh. milioni 46 kutoka shirika hilo.

Alisema wadau hao wanafikisha maendeleo yanayopaswa kufanywa na serikali, lakini kutokana na bajeti kutofika kwa wakati, wanasaidia kuwahudumia wananchi kufikia maendeleo.

Kanali Surumbu alitoa wito kwa halmashauri na wananchi wa Mkinga kuitunza miradi inayofadhiliwa na wadau na kuacha tabia ya kuihujumu kwasababu ni msaada katika kufikia maendeleo.

Meneja wa World Vision Tanzania, Evodia Chija, wakati akiwasilisha taarifa ya miradi waliyoikabidhi serikali, alisema kutokana na changamoto ya upungufu wa matundu ya vyoo katika Shule ya Msingi Tawalani, wamejenga sehemu za kunawia mikono katika Shule ya Msingi Doda ili kuimarisha usafi kwa watoto, hususani kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, Amani Kasinya, aliwashukuru wafadhili na kuwaomba kupeleka miradi hiyo kata zote za wilaya hiyo.

# Wanasiasa waonywa kuitumia Taasisi ya Mwl. Nyerere kimaslahi

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MAKAMU Mwenyekiti wa Taasisi ya Kumbukizi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Peter Mavunde, amewaonya wanachama wa vyama vya siasa na viongozi kuitumia taasisi hiyo kujikweza kupanda kisiasa.

Akiongea na wanachama pamoja na viongozi wa taasisi hiyo Mkoa wa Singida, Mavunde alisema kazi ya taasisi hiyo ni kuisaidia serikali kuwahimiza Watanzania kufanyakazi kwa ajili ya taifa na vizazi vijavyo.

Mavunde ambaye ni Meya mstaafu wa Jiji la Dodoma, alisema kazi nyingine ya taasisi hiyo ni kuwalea vijana wawe na maadili ya kitaifa ili taifa la kesho liweze kuwa imara na linaloenda kwa misingi ambayo hata Mwenyezi Mungu ataibariki.

Aliwakumbusha viongozi wa kwenye nafasi zao za chama na kwamba taasisi hiyo haifungamani na itikadi za kidini, kisiasa, haibagui rangi wala kabila au utaifa.

Mavunde alisema taasisi inawaomba viongozi wote waepukane na aina yoyote ya kuitumia kupata nafasi ya uongozi katika chama cha siasa.

Akiongea kwa njia ya simu kutoka Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Taasisi ya Kumbukizi ya Mwalimu Nyerere, Paul Kimiti, alisisitiza zaidi wanachama wa taasisi hiyo kuenzi falsafa na misingi ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Aidha, alisisitiza kazi kubwa ya wanachama ni kuijenga taasisi hiyo na kuonya kwamba hapatakuwa na nafasi kwa mwanachama anayeivuruga na hatagemei kuona inaleta fedheha kwa Baba wa Taifa na badala yake anataka kuona inaleta heshima kwa mwasisi huyo.

# Viongozi vikundi vya vijana na wanawake wapewa mafunzo

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya CRDB Bank Foundation imeendesha mafunzo ya uongozi kwa viongozi zaidi ya 200 wa vikundi shiriki vya wanawake na vijana katika programu ya IMBEJU.

Mafunzo hayo yamewajumuisha Maofisa Maendeleo wa Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam na mikoa ya Pwani na Morogoro, yakifanyika Makao Makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye semina hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, Tully Esther Mwambapa, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea kwa kuwapatia ujuzi unaohitajika viongozi wa vikundi ili kuongoza na kusimamia vyema vikundi vyao kuendana na mazingira yanayoendelea kubadilika.

"Matarajio yetu ni kuona mafunzo haya yanakwenda kusaidia kuimarisha utendaji wa vikundi vyenu kwa kuwawezesha kusimamia vyema vikundi na kuweka mikakati thabiti itakayosaidia kukua kwa vikundi na wanachama wenu, na baadaye tuwaone mkianzisha kampuni," alisema.

Akielezea mafanikio ya programu ya IMBEJU, Tully alisema hadi kufikia Desemba mwaka jana, CRDB Bank Foundation ilikuwa imetoa mafunzo kwa wanawake na vijana zaidi ya 100,000 sambamba na mitaji wezeshi yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni tano.

Kwenye semina hiyo ya siku moja iliyojumuisha washiriki zaidi ya 200, CRDB Bank Foundation pia ilikabidhi jumla ya mtaji wezeshi wa Sh. milioni 236.57 kwa vijana sita wenye biashara changa walioshiriki mafunzo na mchakato mzima wa ulioandaliwa na Programu ya IMBEJU.

Pamoja na mitaji hiyo, Tully alibainisha kuwa CRDB Bank Foundation inaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwa biashara nyingine za vijana ili kuwapa mitaji wezeshi, pamoja na mafunzo ya utaalamu wa uboreshaji biashara, pamoja na kuwaunganisha na fursa nyingine za kukuza biashara zao ndani na nje ya nchi.

Mwezi uliopita, taasisi hiyo ilipeleka biashara changa tano za vijana kushiriki Kongamano la Biashara Changa Afrika lililofanyika Algeria kujifunza na kuonesha biashara zao. Biashara changa zilizoshiriki ni pamoja na; Mipango App, Niajiri, Lipa kwa Uhakika, Simply Tech, na Settlo.

"Mwaka huu pia tutafungua dirisha la maombi kwa biashara changa za vijana, niwaombe vijana wote wachangamkie fursa hii pindi itakapotangazwa," alisema Tully huku akibainisha kwa upande wa uwezeshaji kupitia vikundi mwaka huu taasisi hiyo inakwenda kuanzisha mikopo ya vikundi.

Akifungua mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa CRDB Bank Foundation, Martin Warioba, aliwataka viongozi wa vikundi kwenda kuyatekeleza kwa vitendo mafunzo hayo katika maeneo hayo ili kuongeza ufanisi, huku akiwaomba kuwa mabalozi wazuri wa IMBEJU kwa kufikisha elimu ya programu hiyo kwa wananchi wengi ili na wao wanufaike na fursa za uwezeshaji zinazotolewa.

Warioba aliwahahikishia washiriki wa mafunzo hayo kuwa bodi yake itaendelea kutunga na kusimamia sera zitakazosaidia taasisi hiyo ya CRDB Bank Foundation kutekeleza uwezeshaji wanawake na vijana ili kusaidia kujenga ujumuishi wa kiuchumi na kuleta ustawi kwa jamii. Akikabidhi mitaji kwa biashara changa za vijana, Warioba aliwataka vijana waliokabidhiwa mtaji wezeshi kwenda kuitumia kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuwa mafanikio watakayopata, yataonesha matunda ya imani iliyonayo Taasisi ya CRDB Bank Foundation kwa kundi hilo mahsusi nchini.

Mapema wiki hii, CRDB Bank Foundation makubaliano ya miaka mitano na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kushirikiana katika maeneo kadhaa na programu ya kwanza ikiwa ni uwezeshaji wa vijana na wanawake.



Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma 'MwanaFA' (kushoto), akitoa mkono wa shukrani kwa Amina Waziri, Mkazi wa Kata ya Mpapayu kwa mchango wake wa kutoa eneo la ekari 7 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya sekondari Kata ya Mpapayu, wilayani Muheza, ambayo imezinduliwa juzi. Wa pili Kushoto ni Katibu wa CCM Muheza, Simoni Leng'ese. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Halotel yamkabidhi gari mshindi wa kampeni yake

**Na Zuwena Shame**

IKIENDELEA na sherehe za maadhimisho ya miaka minane tangu kuanzishwa kwake nchini, kampuni ya mawasiliano ya simu ya Halotel Tanzania, jana ilikabidhi zawadi kubwa ya gari aina ya Mazda CX5 kwa mshindi wa kampeni yake iliyopewa jina la 'Kivumbi na Halotel'.

Kampeni hiyo iliyodumu kwa miezi mitatu kuanzia Oktoba mwaka jana, ililenga kutoa zawadi kwa watumiaji wa mtandao huo kama sehemu ya kurudisha shukrani kwa wateja wake.

Wakati wa kukabidhi gari hilo kwa mshindi katika duka la Halotel lililoko Pam Village, Mikocheni, wilayani Kinondoni, Mkuu wa Kitengo cha Biashara Halotel, Abdallah Salum alisema kampuni hiyo inajali na kuthamini wateja wake.

Alisema kutolewa kwa zawadi hiyo ni mwendelezo wa sherehe za maadhimisho ya miaka minane tangu kuanzishwa kwa huduma za kampuni hiyo nchini.

"Tumeona ni vema kutoa zawadi mbalimbali kwa wateja ili tufurahi nao pamoja maana wao wana mchango mkubwa katika kukua kwa mtandao wetu, hivyo sisi kama Halotel tunalitambua hilo na tunalithamini sana.

"Na leo (jana) hii tunathibitisha hilo kwa kukabidhi zawadi hii ya gari kwa mshindi wa kampeni yetu ya 'Kivumbi na Halotel'," alisema Salum.

Salum aliongeza kuwa Halotel itaendelea kutoa huduma bora kwa gharama nafuu kuhakikisha kunakuwa na urahisi wa upatikanaji huduma za mawasiliano nchini ili kila Mtanzania atumie huduma za kampuni hiyo "kwa sababu kuna furaha".

Baada ya kukabidhiwa zawadi hiyo, Kassim Mbufu, mtumishi mstaafu, alisema amefarijika kushinda zawadi hiyo na kuwataka Watanzania kuendelea kutumia mtandao wa Halotel kwa sababu huduma zao ni nzuri na nafuu.

Kwa kipindi chote cha kampeni ya 'Kivumbi na Halotel', kulikuwa na zawadi za washindi wa wiki, zikijumuisha simu za mkononi, laini za simu za kampuni ya Halotel, vifaa vya kuwezesha mawasiliano na vocha za Sh. 5,000 zilizotolewa kwa washindi 165.

# Waipongeza serikali mazingira rafiki ya uwekezaji Tanzania

**Na Halfani Chusi**

JITIHADA za serikali kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji, zimepongezwa na kampuni za mawasiliano ya simu na teknolojia, zikisisitiza zimeamua kushirikiana na serikali katika kukuza sekta ya mawasiliano nchini.

Jijini Dar es Salaam juzi, Mkuu wa Kitengo cha Mauzo wa Kampuni ya Samsung, Mgope Kiwaga aliipongeza serikali kwa jitihada hizo wakati hafla ya uzinduzi wa simu janja za kisasa za kampuni hiyo.

Alisema kampuni hiyo ya simu imekuja na simu za kisasa ambazo zitaimarisha na kurahisisha njia ya mawasiliano na kurahisisha shughuli za Watanzania za uzalishaji mali.

"Tunaiwezesha dunia kwa njia ya mawasiliano ya kisasa zaidi kwa kutumia simu za mkononi ambayo ubunifu wake unachochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi," alisema.

Alisema Serikali ya Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kubadilisha hali ya uchumi wake kwa kufungua milango ya teknolojia mpya ya mawasiliano na kuweka mikonga ya haraka zaidi kimtandao ili kuwezesha wananchi kuendesha maisha yao kupitia simu za viganjani.

"Simu mahiri ambayo imezinduliwa leo (juzi) ina akili ya bandia ambayo hufungua njia kwa watumiaji kuitumia kama nyenzo ya kila kitu katika maisha yao ya kila siku kuanzia lugha, kujua eneo la kijiografia, kufika mahali na ujuzi mwingine wa kiufundi," alisema.

Aliendelea kusema kuwa Samsung ina mawakala zaidi ya 100 kote nchini wenye uwezo wa kutoa huduma bora kwa wateja huku wakisambaza bidhaa mpya ya kibunifu katika soko la Tanzania.

Mwakilishi wa kampuni hiyo nchini, Manish Jangra alisema simu mpya waliyozindua inaweza kutafsiri kwa njia mbili kwa maandishi na sauti na kuwawezesha watumiaji kuwasiliana kwa urahisi kwa lugha tofauti kwa kutumia mkalimali kwenye simu.

Fahad Fuad, Balozi wa Samsung, alisema simu janja hiyo ya mkononi itawawezesha kuwa na mabalozi wa wazuri kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo nchini kama vile Hifadhi za Taifa Serengeti, Mikumi na Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro, zote zikiwa miongoni mwa hifadhi bora duniani.



# Taasisi za fedha zawafutia mikopo waathirika maporomoko Hanang'

**Na Mwandishi Wetu,** HANANG'

WAFANYABIASHARA wadogo ambao ni waathirika wa maporomoko ya tope wilayani Hanang' mkoani Manyara wamefutiwa mikopo yao kutoka katika taasisi mbili za fedha.

Taasisi zilizofuta mikopo hiyo yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 22 na kutangaza msamaha, ni Vision Fund Tanzania na Metro Life Assurance.

Jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Fedha ya Vision Fund, Chilala Hakoom, alisema dhamira yao imelenga zaidi kuisaidia jamii ya eneo hilo kurudi katika hali ya kawaida na kuziwezesha familia kupitia huduma za kifedha.

Alisema taasisi hiyo inatambua ugumu wa fedha unaotokana na waathirika hao, hivyo imelazimika kufuta mkopo kwa wadeni walioathirika kupitia huduma yao ya Banc Assurance.

Katika msamaha huo, taasisi hizo pia zimetangaza msamaha wa marejesho ya miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu.

Baada ya kutangazwa ahueni hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Janeth Mayanja, aliwataka wadau hao kuendelea kuboresha ushirikiano kati yao, serikali na jamii katika mambo mbalimbali wakati wa shida na raha. "Jumla ya wafanyabiashara 11 wamapata athari katika biashara zao ambao sita wamewafutia mikopo kabisa, hawatalipa na watano wamesahemewa marejesho miezi mitatu, wataaanza kulipa marejesho rasmi Aprili mwaka huu," alisema Mayanja.

Alisema kwa kufanya hayo, wametambua uhalisia wa taasisi yao kwa kujali wateja wao katika kipindi hiki kigumu kwa kutoa msaada wa haraka na ni muhimu kwa wafanyabiashara hao.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Metro Life Assurance, Amani Boma, alisema wanajukumu ya kushiriki katika jambo hilo kwa sababu wanahusika na majanga.

"Ni wajibu wetu kuungana na kushirikiana na serikali katika masuala ya majanga na bima kushiriki kwa wakati na Watanzania mnapaswa kuwa na bima ili ziwasaidie wakati wa matatizo," alisema Boma.

Kwa upande wa mfanyabiashara kutoka Katesh, Fura Massawe, ambaye ni mwathirika wa maporoko hayo alishukuru VisionFund kwa kutambua changamoto zinazowakabili kwa sasa ikiwamo kupoteza mali zilisombwa na maji.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (kushoto), akikaribishwa na kiongozi wa kimila Alais Koina kwenye Kijiji cha Kimotorok, Kata ya Loiborsiret, baada ya mifugo 800 iliyokamatwa na Hifadhi ya Taifa ya Tarangire kuachiwa juzi. Wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Dk. Suleiman Serera. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali yashusha gharama uwekezaji kwa wazawa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI imeshusha gharama zinazotozwa kama kiwango cha fedha za uwekezaji kwa wazawa, kutoka Dola za Marekani 100,000 hadi kufikia 50,000.

Kiwango hicho ambacho ni sawa na Sh.milioni 125 za Tanzania, kinalenga kuwavutiwa wawekezaji wa ndani kuwekeza na kusajili miradi yao.

Meneja Uhamasishaji na Uwekezaji wa Ndani wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Felix John, aliyasema hayo jana wakati akizungumza jijini Arusha.

Alisema wako kwenye kampeni ya kitaifa kuhamasisha uwekezaji wa ndani. John alisema kampeni hiyo imelenga kutekeleza malengo makuu mawili ikiwamo kutoa elimu kwa Watanzania kuhusu dhana ya uwekezaji pamoja na kuwahamasisha kushiriki kikamilifu kwa kuwekeza katika miradi mbalimbali ya kiuchumi na kuchangamkia fursa zilizoko.

"Pia kampeni hii imelenga kubadili fikra za Watanzania wakidhani uwekezaji uko kwa ajili ya wageni kutoka nje ya nchi hivyo kupitia kampeni tunawahamasisha washiriki kikamilifu kutumia fursa zilizotolewa na serikali kupitia sheria mpya ya uwekezaji ya mwaka 2020 ambayo imeshusha kwa kiwango cha chini cha mtaji kutoka Dola za Marekani 100,000 hadi kufikia 500,000 sawa na Sh. milioni 125," alisema.

Aidha alisema mwekezaji huyo wa ndani kwa namna nyingine haitajiki kuwa na kiasi hicho cha fedha ila akiwa na rasilimali ikiwamo ardhi, jengo, mitambo na mashamba anaweza kuwekeza.

"Utaratibu wa kusajili miradi kwa sasa umerahisishwa lakini serikali kupitia TIC imeanzisha kituo cha kutolea huduma mahala pamoja na taasisi 12 za serikali zinazohusika katika mchakato wa kusajili miradi ya uwekezaji hapa nchini kwa ajili ya kurahisisha utaratibu wa kusajili miradi na kutoa huduma kwa wawekezaji ," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni ya Hanspaul inayotengeneza magari ya utalii, ambaye ni mwekezaji wa ndani, Satbir Singh Hanspaul, ameipongeza serikali kwa kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji kwa wawekezaji.

Alisema tangu Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, alipoingia madarakani amejitahidi kwa kiwango kikubwa kuweka mazingira rafiki ya kuwekeza hapa nchini.

Alisema: "Nashukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya kuwekeza kutokana na mabadiliko yalivyo ikiwamo kuweka utaratibu mzuri kwa wazawa kuwekeza hapa nchini na itakuwa chachu ya kuwavutia wageni kutoka nje kuja kuwekeza Tanzania na itachangia kukuza uchumi wa nchi".

# Mil.200/- kugharamia ujenzi jengo mama, mtoto

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imetoa Sh. milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Kituo cha Afya cha Themi.

Ujenzi wa jengo hilo utawaondolea adha wakazi wa eneo hilo waliokuwa wakipata huduma ya kujifungua nje ya kata yao.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Kamati ya Usimamizi wa Kituo cha Afya cha Themi, Melace Kinabo, alisema kilio cha muda mrefu cha wananchi hao kimesikika na serikali imeamua kutatua tatizo hilo.

"Katika kata yetu ya Themi, kumekuwapo na tatizo kubwa la muda mrefu kwa wanawake kukosa huduma ya kujifungua, kiasi kwamba inawalazimu kuhama makazi ili kusogea karibu na huduma.

...Ila kwa sasa, tunaishukuru serikali, kwa kulitambua hilo na kutoa fedha kupitia jiji letu, kwa ajili ya ujenzi wa jengo la mama na mtoto, ambalo litakuwa na wodi ya wazazi na chumba cha upasuaji."

Alisema kuwa mchakato wa ujenzi wa jengo hilo wameuanza miaka mitatu iliyopita na wanashukuru kupata ushirikiano wa serikali, kwa sababu ya changamoto za kujifungua, zilikuwa ni kubwa kutokana na umbali wa kufuata huduma hiyo.

Alisema katika kikao walichokaa, kamati hiyo wamekubaliana kuanza mchakato wa ujenzi huo ikiwamo kutangaza tenda na wamepanga ifikapo Machi mwaka huu, ujenzi wa jengo hilo uwe umeanza mara moja.

"Fedha hizo tayari zimeshaingia kwenye akaunti ya kituo na leo tumefanya kikao cha uamuzi namna ya kutumia fedha hizo na tumekubaliana matumizi sahihi ya fedha za serikali na hatutachelewesha mradi huu na tutakuwa tukishirikiana na Jiji la Arusha ili kuharakisha mradio huo," alisema.

Kinabo aliwaambia wananchi wa kata hiyo kuwa wavumilivu wakati mchakato wa ujenzi unafanyika na wanatarajia ifikapo katikati ya mwaka huu jengo hilo liwe limekamilika.

Aidha, mjumbe wa kamati hiyo, Catherine Nyabamba, aliishukuru serikali kwa kuwapatia fedha za ujenzi wa jengo hilo, kwani litaokoa maisha ya kinamama wanaojifungua ambao hapo awali walipata changamoto kubwa.

Alisema wananchi watanufaika na mradi wa jengo hilo pindi litakapokamilika na kuwapunguzia gharama walizokuwa wakizitumia wakati wa kuwapeleka wake zao, kupata huduma za kujifungua hasa nyakati za usiku.





# Bashungwa awa mbogo makaravati kubomoka

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amekuja juu kuhusu miundombinu ya Barabara ya Kanyinabushwa-Mbale 'A' iliyopo wilayani Missenyi Mkoa wa Kagera kujengwa chini ya kiwango na kusababisha makalavati kubomoka.

Waziri Bashungwa amefikia hatua hiyo kufuatia kipande cha video kinachosambaa mtandaoni kuonyesha mwananchi akilalamikia ujenzi wa barabara na makaravati kujengwa chini ya viwango na kubomoka baada ya muda mfupi.

Taarifa iliyotolewa jana na Wizara ya Ujenzi imemnukuu Wazari Bashungwa akiagiza Bodi ya Usajili ya Wahandisi (ERB) na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) kufika haraka katika ujenzi huo na kumchukulia hatua za kisheria mkandarasi na msimamizi kwa kuhujumu mradi.

Alisema serikali haiwezi kuvumilia makandarasi wasiofuata sheria na taratibu za ujenzi wa miundombinu kwa kuwa wanahatarisha maisha ya watu.

Bashungwa alisema makandarasi na wahandisi wanatakiwa kuhakikisha wanajenga miundombinu kwa kuzingatia viwango kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi za Watanzania. Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Kagera, Avith Theodory, alisema barabara hiyo ilikosa usimamizi ili kuzuia watu kuendelea kupita wakati wa matengenezo na kusababisha makaravati hayo kubomoka. Kwa muibu wa Theodory, mkataba unamzuia mkandarasi kufanya kazi bila kumjulisha meneja mradi, lakini mkandarasi huyo alikiuka sheria.

Alisema TARURA hawalikubali karavati hilo na kumwelekeza mkandarasi huyo kurudi kwenye eneo la ujenzi kurekebisha dosari zilizojitokeza.



Daktari kutoka Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Sigfrid Shayo, akimpima mgonjwa shinikizo la damu (BP) wakati wa kambi maalumu ya siku tano ya upimaji na matibabu ya moyo ijulikanayo kama Mhe. Samia Suluhu Hassan Outreach Services inayoendelea katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa Tabora. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaombwa kukarabati daraja

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SERIKALI imeombwa kukarabati daraja la Mazinge mkoani hapa ili kurejesha mawasiliano ya barabara na kunusuru maisha ya wananchi.

Ombi hilo limetolewa na baadhi ya wakazi mjini hapa kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha mkoani hapa kusababisha kukatika na kuzua hofu kwao na wanafunzi kusombwa na maji.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi juzi katika daraja hilo, wakazi hao walisema endapo daraja halitafanyiwa matengenezo linaweza kusababisha maafa kwao na wanafunzi.

Mmoja wa wakazi hao, Joseph Machiya, aliiomba serikali itengeneze daraja hilo ili waweze kupita na kunusuru maisha ya watoto wao wakati wa kwenda shule.

Gudeha Chambalo, alisema wamekuwa wakipata shida kupita kwenye daraja hilo wakati wa kwenda mjini kufuata mahitaji muhimu.

Dereva bodaboda, Joseph Mahona, alisema wamekuwa wakipata shida kupita kwenye daraja hilo, huku wananchi wengine wakipita juu ya reli na kuhatarisha maisha endapo treni itatokea.

Meneja Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Shinyanga, Samson Pamphiri, alisema miundombinu mingi ya barabara na madaraja imeharibiwa na mvua zinazoendelea kunyesha nchini.

Pamphiri alisema wanasubiri bajeti ipite na mvua kupungua ili waanze kufanya ukarabati wa miundombinu ambayo imeharibika.

# Mamalishe Shinyanga wataka ruzuku kwenye gesi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMALISHE wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuweka ruzuku kwenye gesi inayotumika kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ili kuondokana na matumizi ya mkaa, kuni na kuhifadhi mazingira nchini.

Walitoa ombi hilo juzi katika kongamano la Mwanamke Shupavu lililofanyika katika Kata ya Ukune kwa lengo la kuwajengea uelewa wa masuala ya kiuchumi, afya, ukatili wa kijinsia kwa watoto na wanawake na biashara. Mmoja wa wajasiriamali hao, Tausi Mshima, alisema ili kuondokana na matumizi ya kuni, serikali inatakiwa kuweka ruzuku kwenye nishati hiyo kama ilivyofanya kwa mafuta ya petroli ili kuondoa matumizi ya mkaa kwa kuwa yanahatarisha kutoweka kwa misitu na uharibifu wa mazingira.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Hadija Kabojela, alisema wameanza kutoa elimu ya matumizi ya nishati mbadala ya gesi majumbani kwa wananchi ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji ovyo miti iliyopo kwenye hifadhi ya pori la Usumbwa na hifadhi ya Taifa ya Kigosi Moyowosi.

Alisema wamegawa mitungi ya gesi 100 bure kwa mamalishe na 50 kwenye vituo vya afya na zahanati yenye thamani ya Sh.milioni 3 kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo ambayo ni rafiki kwa mazingira. Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani aliahidi kupeleka hoja hiyo kwa Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu, Dk.Doto Biteko ili kuwapunguzia wananchi gharama ya matumizi ya gesi hasa vijijini.



Ukurasa 12

**UMOJA MPYA WA MAKANDARASI...**

Waanza kazi na kilio cha mfumo wa malipo, kodi na dhamana za kazi zao




Ukurasa 13

Ruzuku kwa vyama vyote vya siasa, hapana sikubali!



Ukurasa 14

**UTT yanadi mapinduzi yake 2023, mauzo hisa yafike masafa ya mbali**

BUFE

IJUMAA JANUARI 19, 2024

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

UCHUMI

# Mwaka mpya na mwelekeo safari yake Rais, njia ijayo ya Dira 2050

**Na Mwandishi Wetu**

NI kawaida kila mkuu wa nchi anapoingia madarakani, huwa na malengo yake na wananchi humfuatilia kwa makini. Naye ana wajibu kuyataja na wakosoaji wanafanya yao, hali hadhalika wapo wanaomkubali wanampigia makofi na kubwa zaidi, inakuwa somo kwa kizazi kijacho.

Kitaaluma, hayo yanaingia katika nadharia, vilevile historia. Darasa la Kumbukumbu na Historia, Sayansi ya Siasa, Demokrasia na Uchumi wa Maendeleo huanzia hapo.

Ni mwezi uliopita, nchi ikitimiza miaka 62 ya uhuru, kwenye usukani kusukuma kwa awamu ya sita, Daktari Samia Suluhu Hassan, amekalia kiti hicho miaka mitatu kasoro sasa ana yake kwa umma.

Katika hotuba ya miaka 62 ya Uhuru wa Tanzania, Rais Dk. Samia, akatekeleza wajibu wake kwa umma akiainisha nchi anakoipeleka, kutoka alikoifikisha katika orodha ya mafanikio.

Kimaendeleo akaanza na msamiati wa kisomi "kufungamanisha ukuaji wa uchumi na sekta za uzalishaji..." lengo ni kupunguza au kufuta kabisa chagamoto za maendeleo zilizoko.

Ni matamshi anayoainisha, pia safari ya kuzindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, Dk. Samia akieleza utashi na mkakati wake umo katika sekta za uzalishaji kuimarishwa, ikiwamo katika eneo lake kipenzi la kilimo, kasi ya uzalishaji wenye tija ufanyike, kuvuka iliko sasa. Alishaanza na kilimo biashara.

Pia akasisitiza ambako hachoki 'kupigia debe kuimarishwa ushiriki wa sekta binafsi ndani na nje ya nchi, kuwafanya wenyeji wawe tayari wa kupokea na kushirikiana na wageni kuwekeza.



Vijana wasomi waliojiunga na mradi maalum wa kilimo cha kisasa mkoani Dodoma, hata kuwaonyesha 'kinalipa' na kuajiri, uliobuniwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. **PICHA: MTANDAO**

Ni ubia wa sekta binafsi na umma (PPP) ulioundiwa sera na sheria tangu Serikali ya Awamu ya Tatu, Dk. Samia akiitumikia kama waziri.

Rais Dk. Samia anaelekeza utashi wake katika dira mpya kuelekea Tanzania ya mwaka 2050, kuwapo ongezeko la pato la kila mwananchi kufikia Dola za Kimarekani 3,000 kwa mwaka, sawa na shilingi 7,545,000, ambacho hakikufikiwa na dira ya sasa inayokoma 2025.

Hapo Rais akijielekeza katika ufafanuzi wa kisomi, kwamba "... kushindwa huko kulisababishwa na ukuaji wa uchumi kutojielekeza kwenye sekta zinazogusa maisha ya watu wengi, hivyo umaskini vijijini haujapungua kwa kasi iliyotarajiwa."

Kimsingi, zikirejewa takwimu ni wastani wa theluthi mbili ya Watanzania wanaishi vijijini, hivyo kunapofanya kubaki mahali wanakoishi wananchi wengi zaidi, hata tafsiri ya hali ya maisha ya Mtanzania inaanzia huko.

Inapoambatanishwa na hilo, moja ya vigezo kuongeza kasi ya maendeleo ni kuwapo kasi kubwa ya uwekezaji, kazi inaonyendeshwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC), chini ya Waziri wa Mipango na Uwekezaji, katika Ofisi ya Rais.

Kisiasa, kiuchumi, mipango na sura pana ya maendeleo, mtaji wa 'amani na utulivu' uhitajika sana kuvutia wawekezaji, eneo mojawapo muhimu ambalo Tanzania inapigiwa makofi na wawekezaji, pia vyombo vya kimataifa.

Ni eneo ambako katika utashi wake, Rais Dk. Samia anapatolea neno kwamba, ni muhimu taifa kuwa na watu mahiri, makini na waadilifu, ili kupata jamii inayochukia rushwa na watiifu katika ulipaji kodi.

Vile vile, Rais Dk. Samia akatoa wito kwa Watanzania ndani na nje ya nchi (Diaspora) kushiriki kutoa maoni katika kuandaa Dira ya Taifa ya Maendeleo kupitia njia za kisasa, kuifanikisha dira mpya ya maendeleo inayokaribia kuanza.

### MTEKELEZAJI MKUU SERIKALINI

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kupitia hotuba zake anataja mafanikio ya miradi ya maendeleo ya serikali anayotumikia, akiorodhsha kama reli, viwanja vya ndege,

**INAENDELEA UK.14**

FEDHA

UMOJA MPYA WA MAKANDARASI WAJA NAYO...

# Waanza kazi na kilio cha mfumo wa malipo, kodi na dhamana za kazi zao

• Wadai baadhi makandarasi wazawa, 'si wazawa'

**Na Beatrice Philemon**

KATIKA kufanikisha mfumo wa ushirikiano wa sekta binfasi na umma, makandarasi wa ujenzi wametoa mapendekezo wanayoamini yakifanyiwa kazi na Wizara ya Ujenzi, kutokuwapo mapinduzi katika sekta hiyo nchini.

Maeneo wanayoyahitaji kufanyiwa yanatajwa kuwa ni kukuzwa uwezo wa makandarasi wa ndani, pia kuleta mapinduzi katika sekta ya ujenzi na tafsiri ya 'makandarasi wazawa' kwenye malipo, kodi, vigezo vya zabuni (Evaluation Criteria) na dhamana za bima.

Ni uwasilisho kwenye uzinduzi wa Chama cha Umoja wa Makandarasi na Watoa Huduma Shirikishi Tanzania (TUCASA), Mwenyekiti Samuel Marwa, akilalamika baadhi wanaitwa 'makandarasi wazawa', lakini katika uhalisia hawakidhi sifa za kuwapo katika kundi hilo.

Hapo ndio Mwenyekiti Marwa, anashauri Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) iwe na tafsiri mpya tofauti na inayotumiwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), ikiegema hisa zilizoko kwenye kampuni, akidai sahihi.

"Kwa CRB 'local contractor' awe yule ambaye asilimia 100 ya hisa ni za wazawa. Hii haitawanyima wageni kazi, lakini wasinufaike na fursa za upendeleo wa wazawa, ili kuleta ushindani wa haki.

"Tusiendelee kupotosha takwimu katika soko, upunguze kuvuja kwa uchumi na kuendeleza ukuaji wa makandarasi wa ndani," anaeleza Marwa.

### UNDANI WA MALIPO

Anasema Umoja wa Makandarasi wamefanya utafiti mdogo nchini na kugundua zaidi ya asilimia 93 na walikumbana na ucheleweshaji malipo, pia asilimia 92 ya waliocheleweshewa, hawakulipwa riba kama ilivyoainishwa kimkataba.

"Malipo ni kipengele cha lazima katika kukua kwa mkandarasi. Hatuwezi kusema tunakuza wazawa, ikiwa hatutaweka mikakati ya kuwalipa kwa wakati," anasema Marwa.

Anasisitiza kulipwa kwa wakati kunawezekana, iwapo kila mkataba utaandikwa pale malipo yametengwa fedha mahsusi (ring fenced) kwa mkataba huo, jambo analilotaja liliwezekana kwa vipindi fulani kiserikali.



Barabara ya lami, zao la ufundi wa mkandarasi wa ujenzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **"Tusiendelee kupotosha takwimu katika soko, upunguze kuvuja kwa uchumi na kuendeleza ukuaji wa makandarasi wa ndani.**



Shughuli za ujenzi zikiendelea chini ya mkandarasi.

Aidha, anataja malipo yanapaswa kusimamiwa na kisheria, hali inayomzuia mwenye kazi asiingie mkataba na mkandarasi, iwapo hana fedha.

Eneo lingine analitaja ni kwa watoa huduma kupunguza kiasi kikubwa cha gharama za ujumla za ujenzi, akitaka nalo hilo lifanyiwe kazi na anashauri, akiani likifanyika kwa miradi yote, itasaidia kuokoa fedha nyingi katika mradi.

"Kwa mfano, nchi ya Uingereza ina Sheria ya 'Housing Grants, Construction and Regeneration Act' (HGCRA) inayolazimisha malipo ya kila mwezi kwa makandarasi na utafiti unaonyesha kuwa miradi mingi sana inakamilika kwa wakati na kwa gharama nafuu zaidi, kuliko ilivyokuwa kabla ya sheria hii kuanza kutumika," anaeleza.

Marwa anataja namna rahisi ya kutatua tatizo ni kuwa na uhakika wa malipo ya makandarasi kwa muda sahihi na gharama nafuu.

### MAKANDARASI NA KODI

Katika kodi, anakitaja kipengele kinachomrudisha nyuma kukua kwa makandarasi ndani, akifafanua kiitwacho 'tax point' mlipaji anatakiwa kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), mara mtu unapopeleka hati ya madai kwa mwenye kazi, hata kabla hajalipwa.

Katika hilo, Mhandisi Marwa analalamika kwamba, kodi hiyo ingekusanywa wakati mkandarasi analipwa, kwani kinachofanyika sasa kulipa kabla, wao wanaona ni changamoto, kwani katika uhalisia, humchukua hata miaka miwili kwa makandarasi kulipwa.

Analitaja kuwa eneo linalopaswa kuangaliwa upya na serikali, hususan kwenye biashara ya ukandarasi, maana iko tofauti na mauzo ya bidhaa zingine.

"Hapa mkandarasi ananunua vifaa na kulipa mafundi kwa niaba ya mwenye kazi (hununui kuuza), ili akishajenga kama ni ukuta wa nyumba, arejeshewe, aendelee kununua vifaa vingine.

"Ukimkata VAT hata kabla hajalipwa, unazidi kumpunguzia nguvu ya kuendelea kufanya kazi, ingekuwa haki kama angelipa VAT, baada ya kuikusanya kutoka kwa mlipaji," anasema.

Pia anataja Kodi ya Zuio (Withholding Tax - WHT), hawaridhiki inavyotekelezwa, akisema makandarasi wana mtazamo kwamba inapaswa kutatuliwa, tatizo hili kwenye kamati iliyoundwa na Waziri wa Ujenzi, akianika maoni yake kuwa:

"Tunaamini atakufikishia mapendekezo hayo kwa waziri na ombi letu ni kwamba utekelezaji wa ukusanyaji wa 'WHT' (kodi ya zuio) urejewe na kurekebishwa kama tulivyoshauri ili ufanyike kwa haki.".

### VIGEZO ZABUNI/BIMA

Marwa akifafanua kuhusu vigezo vya zabuni vilivyopo, anasema baadhi ya vinavyotolewa kupata kazi ni kikwazo kikubwa katika ukuaji wa makandarasi wa ndani.

"Vigezo vingi tumeiga kutoka Benki ya Dunia na hizo 'multilateral banks' ambavyo vinakidhi nchi na mataifa yote duniani.

"Hivi vinatuchukulia makandarasi wote na watoa huduma kama tunalingana dunia nzima, kwa hiyo kwa njia hii 'Heavy Weight' (bondia uzito mkubwa) anapangwa kupambana na 'fly weight' (uzito wa kati. Hivi kuna haki hapo?" anauliza.

Katika nafasi ya bima, Marwa anasema taasisi nyingi za umma hazikubali dhamana za bima, zinahitaji benki na kulazimu mkandarasi azuie kiasi kikubwa cha fedha, kwa ajili ya dhamana hizo mwanzoni tu wa mradi.

Hicho anakitaja ni kikwazo katika ukuaji makandarasi nchini, kwani anaposhindwa kukidhi kigezo anakwama, wakati mbadala wa dhamana za bima wanaamini ina nafasi kwa manufa aya pande mbili za mkataba wa ujenzi.

Marwa anasifu kwamba biashara ya bima kwa sasa inasimamiwa vizuri nchini na misimazi wake, TIRA inaaminika kimataifa.

"Kwa kuwa gharama zake ni nafuu kuliko benki na kuna urasimu mkubwa kukidhi matakwa ya benki kuliko matakwa ya bima," anasema.

Lingine analolamikia kuambatanisha na bima, ni kwamba mtiritriko huo wanaoshirikiana kibiashara, huwa hawana uhakika wa kulipana na imekuwa kikwazo kwa makandarasi wadogo.

Rai yake ni kwamba, wasilazimishwe dhamana za benki, bali mkandarasi aachwe achague kama ni benki au bima anayopaswa kuingizwa katika mikataba ya umma (PPRA Standard Forms of Contract).

### TAKWIMU ZA UJENZI

Marwa anasema hadi sasa zinaonyesha makandarasi wa ndani wanafanya kazi nyingi na zenye thamani kubwa, kuliko zamani.

"Ukipitia kwa juu juu utaona kwamba zaidi ya asilimia 96 ya makandarasi waliosajiliwa na CRB ni wa ndani na thamani ya kazi wanazofanya kwa sasa zina thamani ya takribani asilimia 53 ya kazi zote za ujenzi," anaeleza na kuendelea;

"Wakati wageni ambao ni chini ya asilimia nne wakifanya kazi zenye thamani ya takribani asilimia 47."

Analalamika kuna takwimu zinazowapotosha watunga sera na sheria, akifafanua: "Kwa mfano kwa 'Mwaka wa Fedha 2022/2023 CRD' ilisajili miradi 4,141 yenyet hamani ya shilingi trilioni 7.62.

"Kati ya hiyo, miradi 4,022 (takribani asilimia 97 ya miradi ilikuwa na thamani ya shilingi trillioni 3.1 (sawa na asilimia 40 ya thamani ya miradi yote) ndiyo tu ilitekelezwa na makandarasi wa ndani."

Anaeleza kuwapo miradi 118, sawa na asilimia tatu, yenye thamani ya shilingi trilioni 4.5 ilitekelezwa na wageni. Kwa hiyo, sehemu kubwa ya fedha shilingi trilioni 4.5 ilienda nje haikuzunguka katika uchumi wa ndani.

Katika nia mojawapo ya kujiimarisha, wao makandarasi wa ndani ndio wameunda Umoja wa Makandarasi na Watoa Huduma Shirikishi Tanzania (TUCASA), kushughulika nyendo na haki zao.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Ruzuku kwa vyama vyote vya siasa, hapana sikubali!






**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

SIKU Msajili wa Hazina (TR), Nehemia Mchechu alipoitisha kikao kazi na wahariri wa vyombo vya habari nchini, kuwaeleza mpango wa serikali kufanyia marekebisho taasisi zake, nilifarijika sana.

Faraja yangu ilikuja pale niliposikia kuwa serikali imeona ina mzigo wa taasisi takribani 300 na hivyo kufikiria kuzipunguza, kwa baadhi kufutwa na zingine kuunganishwa, hususan zenye dhima inayofanana.

Hatima ya yote, ni kupunguza matumizi katika taasisi hizo na serikalini kwa ujumla na kupata uwezo wa kuhudumia wananchi ambao si siri, wanakabiliwa na changamoto lukuki za kimaisha.

Mchechu akatangaza kwamba, kuanzia wakati huo mwaka jana, basi taasisi moja moja ikutane na wahariri na kuelezea majukumu na mipango yake ya baadaye, ili wahariri nao wafikishe ujumbe kwa jamii ili kuielewesha nini taasisi husika inafanya.

Lengo ni kuhakikisha kuwa, endapo hatua itachukuliwa iwe ya kufuta au kuunganisha taasisi, basi wananchi wawe wamejiridhisha na ama kukubaliana au kupingana na uamuzi husika, ingawa hatima yake ni njema.

Taasisi zinaendelea kukutana na wahariri na kujieleza na tayari kuna mwelekeo wa kuona ni zipi zinatakiwa kubaki na zipi kuondoka na zipi ziunganishwe na tayari baadhi zimeshatangazwa na serikali kuhusu hatima yao.

Lakini wakati hilo likiendelea kufariji wengi wanaotaka maendeleo na hasa wasiotaka matumizi makubwa yasiyo na maslahi mapana kwao, kuna mjadala unaendelea kuhusu miswada ya sheria za uchaguzi.

Wadau wamekuwa wakitoa maoni yao kuhusu miswada hiyo iliyokwishawasilishwa bungeni na sasa baada ya maoni, itachambuliwa na kurudi bungeni kujadiliwa kuwa sheria kwa itakayokuwa imekubaliwa.

Pamoja na masuala hayo ya sheria za uchaguzi, baadhi ya wadau wamekuja na mapendekezo ya kutaka vyama vyote vya siasa nchini, vipewe ruzuku kila mwaka, bila kujali vina wabunge au la.

Wanaounga mkono hoja hiyo, wanasema ni vema kufanya hivyo, ili vyama hivyo vijiendeshe na kuondokana na kadhia ya viongozi wenye ukwasi katika vyama hivyo, kuvihodhi na kuwa na kauli kuliko wengine.

Mimi bila kuangalia makunyanzi ya anayeunga mkono hoja hiyo, napingana nayo kwa nguvu kubwa sana, nikirejea alichokianzisha Mchechu kwa taasisi za umma, cha kutaka kupunguza matumizi.

Tatizo ni kwamba, vyama vya siasa baadhi vinachukuliwa kama ujasiriamali na vichaka vya fursa za nafasi na kipato, badala ya kuongoza wananchi kutatua matatizo yao na kujiletea maendeleo.

Zamani vyama vya siasa vilianzishwa kwa madhumuni ya kupambania uhuru kutoka kwa wakoloni, hivi sasa vinaanzishwa kama fasheni ya nami niwe fulani niongoze watu, huku nikijipatia chochote kitu.

Tanzania tuna utitiri wa vyama vya siasa kinyume kabisa na imani aliyokuwa nayo Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye kimsingi alitaka nchi iwe na vyama visivyozidi vinne vya siasa vilivyo imara na makini, vipambane na chama tawala.

Akisema kuwa vyama vya upinzani viwe na nguvu ya kukishitua na kukiamsha chama chenye serikali kinaposhikwa na usingizi na kushindwa kuhudumia watu.

Baada ya mfumo wa vyama vingi vya siasa kurejeshwa nchini mwaka 1992, kila mtu akataka awe na chama kwa ajili ya kumrahisishia kuingia madarakani na kuwa mmoja wa wakazi wa Ikulu.

Matokeo yake ni utitiri wa vyama, vingine vinavyosubiri kuonekana wakati wa uchaguzi na unapomalizika vinarudi mafichoni. Sasa navyo eti vinataka vipewe ruzuku, ili iweje? Wanataka kupeleka wapi hizo kodi za wananchi?

Ningekuwa na madaraka ya kuamua lolote nchini, ningetangaza kufutwa kwa vyama vyote vya siasa na kuwa na mfumo wa wananchi kujichagulia viongozi wao mitaani wanakoishi, na si lazima kuwa na vyama.

Watanzania tusikubali kodi tunazotozwa kwa jasho letu zichukuliwe wapewe watu wasio na masaada kwetu, bali kwa matumbo yao, kwa sababu hata mfumo wenyewe wa siasa unatutumbukia nyongo.

Kwa kuwa madaraka hayo sina na sitayapata hivi karibuni, nashauri ruzuku iondolewe kwa vyama vyote bila kujali vina wabunge au la, na ikiwa lazima viendelee, basi idadi yao ipungue kuanzia mwakani, ili vitakavyobaki viwe vyenye wabunge tu. Mungu atuongoze!

FEDHA

# UTT yanadi mapinduzi yake 2023, mauzo hisa yafike masafa mbali

**Na Frank Monyo**

NI utaratibu malengo huwekwa mwanzo wa mwaka. Katika kipengele hicho wataalamu wa hisa nchini, Taasisi ya Uwekezaji ya UTT AMIS, inasema mifuko ya uwekezaji nchini ni mbadala maridhawa ya kukuza mtaji kwa mtu yoyote, anayetaka kutimiza malengo yake.

Wapo wanaoamini kwamba mwaka 2024 ni wa mafanikio kwa dhana ambayo sio rasmi, kwamba namba za mwaka huo 'zinagawanyika kwa mbili.'

Mkurugenzi Mtendaji wa UTT AMIS, Simion Migangala, anawapa rai Watanzania kuwekeza na taasisi hiyo, kwani katika kipindi cha mwaka mmoja, ukubwa wa mifuko imekuwa kutoka shilingi bilioni 996.5 hadi kufikia shilingi trilioni 1.535, baada ya mifuko ya fedha kufunguka nchinii.

Migangala anaitaja Mifuko ya Uwekezaji ya taasisi hiyo, ambayo: Umoja; Mfuko wa Watoto; Hatifungani; Jikimu; Wekeza Maisha; na Mfuko wa Jikimu.

Anasema kuwa ongezeko hilo la kiasi cha shilingi bilioni 538.9 ni sawa na ziada asilimia 54, ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 383.7. Ongezeko hilo la ukubwa wa mifuko, pamoja na kufunguka mifuko ya fedha anaitaja ni zao la imani ya wawekezaji. Pia, kuna elimu itolewayo kuhusu akiba, uwekezaji na faida shindani kwenye mifuko tajwa.

"Kwa kipindi cha mwaka mmoja, ukubwa wa mifuko umeongezeka kutoka shilingi bilioni 996.5 tarehe 30 Juni 2022 hadi kufikia shilingi trilioni 1.535 tarehe 30 Juni 2023.

"Ongezeko hili la kiasi cha shilingi bilioni 538.9 ni sawa na asilimia 54 ikilinganishwa na ongezeko la shilingi bilioni 383.7, ongezeko hilo la ukubwa wa mifuko linatokana na imani ya wawekezaji kwetu, elimu itolewayo juu ya akiba na uwekezaji pamoja na faida shindani kwenye mifuko," anasema




Mkurugenzi Mtendaji wa UTT AMIS, Simion Migangala akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) kuhusu mafanikio ya mifuko ya taasisi hiyo katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mifuko ya Uwekezaji uliofanyika mwishoni mwa mwaka jana. **PICHA: FRANK MONYO**

Katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Mifuko ya Uwekezaji uliofanyika mwishoni mwa mwaka 2023, Migangala, akautaja Mfuko wa Umoja umeongezeka kwa asilimia 11.2 na Mfuko wa Wekeza Maisha asilimia 12.5.

Mingine anaitaja ni: Mfuko wa Watoto asilimia 12.4; Mfuko wa Jikimu asilimia 14.0.

"Kwa mifuko iliyosalia yenye uwekezaji kwenye maeneo yenye mapato vya kudumu, faida kwa Mfuko wa Ukwasi ni asilimia 12.5 na Mfuko wa Hatifungani ni asilimia 12.3. ikilinganishwa na asilimia 9.7 ya kigezo linganifu," anaeleza.

### UCHUMI VS SOKO FEDHA

Migangala anaeleza kuhusu maendeleo ya Soko la Hisa, kwamba utendaji kwa kampuni za ndani ya nchi unapimwa kwa kuangalia mabadiliko ya Fahirisi (Tanzania Share Index).

Anataja, katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe Juni 30 mwaka jana, Fahirisi imeonyesha kuwa na ongezeko la asilimia 4.1 kutoka 3,928.5 mnamo Juni 2022 hadi 4,091.8 tarehe 30 Juni mweaka jana.

"Hii inamaanisha kwamba, katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2023, bei za hisa kwa kampuni za ndani ya nchi ziliongezeka sawa na asilimia 4.1.

"Kati ya sababu zilizosababisha kupanda kwa bei za hisa ni pamoja na utendaji mzuri wa kampuni za ndani kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, kuongezeka kwa imani ya wawekezaji wa ndani na nje na uboreshwaji wa mazingira ya uwekezaji hapa nchini," anasema

### UTENDAJI WA MFUKO

Mwenyekiti wa Bodi ya UTT AMIS, Casmir Kyuki, anasema katika mpango mkakati wa miaka mitano utakaoishia mwezi Juni mwaka huu, taasisi hiyo imeazimia kujikita kwenye matumizi ya teknolojia katika kutoa huduma kwa wawekezaji.

"Miaka minne iliyopita kampuni ya UTT AMIS ilizindua huduma ya uwekezaji kwa kutumia simu za kiganjani yaani UTT SimInvest (*150*82#), programu ya matumizi (UTT AMIS APP) na inaendelea kuunganisha mifumo ya benki na mifumo ya UTT AMIS.

> **"Hii inamaanisha kwamba, katika kipindi cha mwaka ulioishia Juni 2023, bei za hisa kwa kampuni za ndani ya nchi ziliongezeka sawa na asilimia 4.1.**

'Lengo la uunganishwaji huu ni kuongeza ufanisi kwa kupunguza mlolongo wa hatua za uchakataji wa miamala inayofanywa kwa njia za benki," anasema

Kyuki anaeleza kwamba hadi kufika Juni 30 meaka jana, Meneja wa Mifuko (UTT AMIS) ameunganisha mifumo yake na benki nne, mojwea ikibena jukumu la uangalizi wa mifuko hiyo.

Aidha anataja UTT AMIS inaendelea na kazi ya kuunganisha mifumo yake na benki nyinginezo, sita, husi yale ziokiwa za kigeni zenye makao nchini.

"Ni matumaini yangu kuwa, pindi zoezi hili la uunganishaji mifumo litakapokamilika, litaongeza idadi ya miamala inayofanywa kwa njia ya benki kwa asilimia kubwa zaidi.

"Pia, huduma ya kuuza vipande kwa njia ya simu (SimInvest) imeanzishwa ambapo wawekezaji wanaweza kuuza vipande vyenye thamani hadi ya shilingi milioni mbili. Vilevile, jitihada maalumu zimeanza kufanyika za kuwafikia Diaspora (Watanzania waishio nje ya nchi )," anasema

### MATARAJIO YA 2023/24

Kyuki anasema kuwa kipindi cha miaka minne ya mwanzo ya utekelezaji wa mpango mkakati wa taasisi ya UTT AMIS utakaoishia tarehe 30 Juni 2024, kumekuwapo mafanikio makubwa zaidi ya ilivyotarajiwa.

Taasisi hiyo inaendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mpango huo ikiwamo kuboresha mifuko, huduma kwa wawekezaji na kubainisha fursa nyingine za kibiashara kwa manufaa ya wawekezaji, serikali na wadau wengine.

UTT AMIS inaendelea kuboresha namna ya uendeshaji wa mifuko, ili iwe ya kisasa zaidi na kuhakikisha wawekezaji wanapata faida shindani kuendana na hali ya soko na kutoa huduma bora.

## Mwaka mpya na mwelekeo safari yake Rais, njia mpya ya dira 2050

**INATOKA UK.11**

bandari, huduma za kiuchumi na kijamii, madarasa ya shule, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

"Serikali itahakikisha miradi ya kipaumbele na kimkakati inayoendelea kutekelezwa inakamilika kwa wakati ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi mipya," akatamka Waziri Mkuu, katika kikao cha Bunge, kupitisha bajeti ya mapato na matumizi mwaka wa fedha 2022/2023, jijini Dodoma.

Majaliwa anaahidi Serikali ya Awamu ya Sita itahakikisha miradi ya kipaumbele na kimkakati inatekelezwa na kukamilika kwa wakati, sanjari na miradi mipya.

Anaitaja kuwa ni ya miundombinu; ujenzi wa Reli ya Kisasa kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR); kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere), mtambo ukitarajiwa kuwashwa hivi karibuni.

Pia anataja ujenzi wa viwanja vya ndege na kipaumbele kwa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Chongoleani - Tanga.

Majaliwa amegusa jitihada za kuinua kilimo, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania mtaji wa nyongeza, huku sekta ya maji ikiwa na hatua kubwa ikiwa katika safari ifikapo mwaka 2025, upatikanaji huduma ya maji mijini na vijijini unafika wastani wa asilimia 95.



# Wananchi walalamika soko kutelekezwa miaka tisa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKAZI wa Kata ya Nkuhungu jijini Dodoma wamelalamikia kutelekezwa kwa soko lao kwa kipindi cha miaka tisa, licha ya uwekezaji mkubwa uliofanywa.

Wamesema hali hiyo imesababisha wao kuendelea kufanya biashara maeneo yasiyo rasmi na kuipotezea mapato serikali.

Waliyasema hayo jana wakati wakizungumza na waandishi wa habari kuhusu kutelekezwa kwa soko hilo.

Mmoja wa wananchi hao, Karim Waziri, mkazi wa kata hiyo alisema huu ni mwaka wa tisa soko hilo halijatumika licha ya uwekezaji mkubwa ulifanywa na wananchi.

"Huu ni mwaka wa tisa soko hili halijafanya kazi pamoja na watu kuwekeza miundombinu mbalimbali ikiwamo meza kwa ajili ya kuweka bidhaa hali ambayo inatufanya kuendelea kufanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi.

"Tunaomba serikali iingilie kati soko hili lianze kufanya kazi na sisi kupata eneo la kufanya biashara badala ya kuendelea kukaa kwenye maeneo yasiyo rasmi kama ambavyo hivi sasa wanataka kuanzisha eneo lingine ambalo siyo rasmi ili kuwa soko wakati hili tumelitelekeza," alisema.

Kadhalika alisema licha ya kufuatilia sehemu mbalimbali ili kubaini nini shida hakuna jibu ambalo wamepatiwa kutoka kwa viongozi wao.

"Mkuu wa wilaya alitoa maagizo hapa lijengwe soko la kisasa lakini tunashangaa kabla ya hili ambalo limetelekezwa kwa miaka tisa kuanza kufanya kazi tunasikia pia viongozi wanataka kuanzisha soko lingine jipya eneo ambalo ni la wazi na DC (Mkuu wa Wilaya) alishatoa agizo pale pasifanyike chochote," alisema.

Naye Anjelina Bundala alisema wanashangaa soko hilo kushindwa kuanza kutoa huduma kwa muda wa miaka tisa huku kukiwa na wajasiriamali wengi mitaani ambao wanafanya kazi maeneo yasiyo rasmi.

"Tunaomba watueleze hili soko waliopewa maeneo ya kufanyia biashara ni watu gani kama ni wafanyabiashara kwanini hawapo hadi leo, lakini kama waliwapa watu na hawataki kufanya biashara hapa watupe sisi wenye uhitaji badala ya kutelekeza kwa muda wote huo," alisema.

Lucas Muhede, alisema walishafuatilia kwa uongozi wa Jiji na kupatiwa michoro ambayo ilipaswa kutumika kwenye soko hilo ili kuliboresha, lianze kufanya kazi lakini wanashangaa kuambiwa kuwa linaanzishwa lingine.

"Hili ndilo soko mama ambalo lina vibanda vya biashara 394 na tangu kuanzishwa kwake miaka tisa iliyopita halijawahi kufanya kazi na watu wameendelea kufanya biashara zao maeneo yasiyo rasmi na kuipotezea mapato serikali kwa miaka hiyo," alisema.

Akitolea ufafanuzi kuhusu suala hilo Diwani wa Kata ya Nkuhungu, Daudi Mkandi, alisema soko hilo limeingizwa kwenye mpango wa bajeti ya mwaka huu ili kuboreshwa baadhi ya miundombinu na kuanza kutoa huduma.

"Kweli soko hili kwa muda huo wa miaka tisa limeshindwa kufanya kazi kwa changamoto kadhaa zilizokuwapo ikiwamo umeme lakini leo (jana) tulikuwa kwenye kikao cha bajeti tayari limeingizwa kwenye bajeti kwa ajili ya utekelezaji," alisema Mkandi.

Kuhusu soko jipya linalolalamikiwa kuanzishwa, Mkandi alisema siyo kweli kwani kinachoanzishwa hivi sasa ni stendi kwa ajili ya daladala ambazo hivi sasa hazina eneo maalum.

Mkandi alisema: "Pale ni stendi siyo soko kama ambavyo baadhi ya watu wanapotosha lakini kutakuwa ni vibanda vya huduma mbalimbali ambavyo watavitumia wale ambao tumewatoa barabarani na kuwaleta hapa eneo ambalo ni rasmi".



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Jenifa Christian Omolo na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Maalum ya Wasioona Buigiri, Samwel Jonathan, wakimkabidhi Mwanafunzi wa Darasa la Awali wa Shule hiyo, Zulfat Ibrahimu, kadi ya bima ya afya ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani Dodoma. Wakishuhudiwa na wawakilishi wa viongozi na wajumbe wa Chama cha Wafanyakazi TUGHE tawi la wizara hiyo juzi. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Vibanda 14 kujengwa Soko la Mazao Kibaigwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kongwa imeanza kufanya maboresho mbalimbali katika Soko la Kimataifa la Mazao Kibaigwa ikiwamo kujenga vibanda 14 ili kuongeza mapato ya halmashauri.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Omary Nkulo, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na Nipashe kuhusu uboreshaji wa soko hilo linalotumiwa na wafanyabiashara wa mazao ndani na nje ya nchi.

Alisema wameanza ujenzi wa vibanda kuzunguka eneo la soko hilo kwa lengo la kuongeza mapato na kuimarisha uzio.

Kadhalika, alisema ujenzi wa vibanda hivyo utagharimu Sh. milioni 98 na gharama ya kibanda kimoja ni Sh.milioni saba na kwa awamu ya kwanza wameanza na ujenzi wa vibanda 10 vinavyotarajiwa kukamilika Machi mwaka huu.

Alibainisha kuwa soko hilo limekuwa miongoni mwa vyanzo vikuu vya mapato katika halmashauri hiyo ambapo mwaka jana walikusanya mapato ya Sh.milioni 900.

Kadhalika alisema ili kuimarisha soko hilo wanatarajia kununua mzani mkubwa wa kisasa wa kidijitali kwa sababu uliopo umekuwa chakavu, kwamba gharama za mzani mpya ni Sh. milioni 90.

# Eneo lako likikutwa chafu faini ya 300,000/- itakuhusu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imetangaza kuwatoza faini ya Sh.50,000 hadi Sh.300,000 kwa wananchi watakaokutwa maeneo yao machafu.

Mkuu wa kitengo cha usafi na udhibiti wa taka ngumu wa halmashauri hiyo, Dickson Kimaro, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mikakati wa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu.

Kimaro alisema kuwa ili kuepukana na faini na vifungo wanatakiwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa na maofisa wa afya waliopo kuanzia kwenye kata na mitaa ndani ya Jiji.

"Halmashauri imeweka kiwango cha Sh. 50,000 hadi Sh. 300,000 kwa watakaobainika kukiuka matumizi ya sheria ya afya ya jamii na sheria ndogo," alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa halmashauri kupitia wataalamu wake wataendelea kutoa elimu kwa wakazi wa Jiji ili kujilinda na magonjwa hayo kwa kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha.

Alitaja maneo ambayo yatakayofikiwa na elimu hiyo kupitia kwa wataalamu wake ni pamoja nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa, masokoni migahawa, hoteli, mikusanyiko ya watu, vilabu vya pombe za kienyeji na stendi za daladala na mabasi yaendeayo mikoani pamoja na vibanda vya biashara.

Alisema elimu hiyo itatolewa na wataalamu wa afya kwa kushirikiana na watendaji wa kata, mitaa na madiwani, kwa ajili ya kuwahimiza watu kunawa mikono na sabuni na maji tiririka, chakula kiwe cha moto na wahudumu wa maeneo ya kuuzia vyakula kuhakikisha wamepimwa afya zao.

Hivyo aliwahimiza wafanyabiashara wa matunda sokoni, mitaani na mama lishe hususani wanaotembeza kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo maofisini wahakikishe wanazingatia sheria za afya ili kuepukana na kufungiwa biashara zao na kutozwa faini.



# Kamati yaishauri TARURA miradi kipaumbele

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KAMATI ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imeishauri Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kupeleka bajeti na mapendekezo ya miradi ili kuamua ya kuanza nayo.

Ushauri huo umetolewa na wajumbe wa kamati hiyo juzi wakazi wa ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo wilayani humo.

Wajumbe hao walisema kuwa madiwani wana uelewa juu ya mahitaji ya wananchi wao kwa kuwa ndio wanaoishi nao, hivyo wanapaswa kushiriki kupendekeza miradi hiyo ili kuwaondolea kero.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Bosco Mwanginde, alisema wakati wakiandaa bajeti ya mwaka 2024/25 ni vyema TARURA wakapeleka bajeti yao kwenye vikao vya kamati ya fedha ili wao wapate nafasi ya kushauri barabara ipi ipewe kipaumbele na kuhakikisha bajeti inayopangwa inaendana na uhalisia wa mradi.

Vilevile kamati hiyo imeagiza TARURA kufuatilia agizo la Rais Samia Suluhu Hassan la kuhakikisha barabara zinaelekezwa kwenye maeneo ambayo miradi ya jenga kesho iliyo bora (BBT) itatekelezwa zinafunguliwa ili kutekelezwa kwa ufanisi na kukamilika kwa wakati.

"Niwaombe mlete taarifa inayoonyesha bajeti ya kufungua barabara hizo imetengwa ili kamati hii ipate namna ya kuendelea kufuatilia utekelezaji kama Rais alivyoagiza," alisema Mwanginde.

Akijibu hoja za wajumbe wa kamati hiyo, Meneja wa TARURA wa Wilaya ya Chunya, Emmanuel Kayola, alisema miradi yote inaendelea vizuri, maoni ya mapendekezo na maelekezo yao wameyapokea na kuahidi watayafanyia kazi.

Kamati hiyo imekagua miradi yenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 600 ambayo inasimamiwa na TARURA. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa daraja la Lualaje, daraja la Magunga kupitia barabara ya Ngwala na ujenzi wa Barabara ya Malangamilo yenye urefu wa kilomita nane.

# Fundi ajiua, amwachia ujumbe mjamzito

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

FUNDI ujenzi, Venance Haule (24), Mkazi wa Mtaa wa Idundilanga Halmashauri ya Mji wa Njombe, anadaiwa kujiua kwa kujinyonga kwa pazia na kumwachia ujumbe mwanamke mwenye ujauzito wake amtunze mwanawe baada ya kujifungua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Mahamoud Banga, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo juzi majira ya asubuhi chumbani kwa kijana huyo.

Kamanda Banga alisema kuwa inadaiwa kabla ya kuchukua uamuzi huo, fundi huyo alikuwa akipata usumbufu kutoka kwa ndugu wa mwanamke huyo wa kudaiwa mahari mara kwa mara.

Alisema kana kwamba haitoshi, ndugu hao walikuwa wakimtolea vitisho kuwa wao ni askari polisi na kwamba anatuhumiwa kuishi na ndugu yao huyo wakati akiwa ni mwanafunzi wa sekondari na kusababisha akatishe masomo.

"Sababu kubwa ya kujiua ni suala zima la mapenzi na kwamba yeye alikuwa anaishi na mwanafunzi wa sekondari, lakini aliacha shule mwaka 2022 akiwa kidato cha pili," alisema Banga.

Alisema kutokana na kutohudhuria masomo kwa muda mrefu, alifukuzwa shule na kukosa sifa ya kuendelea kuwa mwanafunzi.

"Lakini kimsingi walikuwa wanakuja kwao watu ambao kwa maelezo ya mwanamke huyo wa maelezo ya binti ni ndugu zake wakijifanya ni askari wakimtishia wamefungua kesi kituo cha polisi kuwa anaishi na mwanafunzi, lengo lao kubwa lilikuwa awape fedha za hongo au mahari," alisema.

Kamanda huyo alisema hivi karibuni ndugu hao walifika nyumbani kwa fundi huyo na kumchukua ndugu yao huyo na kumrudisha nyumbani ikiwa ni kushinikiza walipwe mahari.

"Kijana shughuli zake kubwa zilikuwa ni ujenzi kwa hiyo uwezo wake ulikuwa sio mkubwa kifedha katika hali kama hiyo alikuwa anampenda mwanamke huyo kwa maelezo aliyoacha kwenye ujumbe kwamba huyo mwanamke ni mjamzito na mtoto atakayezaliwa amtunze," alisema Banga.

Akizungumza na Nipashe, mmliki wa nyumba aliyokuwa amepanga fundi huyo, Sarah Magehema, alisema aliishi kwa kipindi cha miezi sita na mwanamke huyo na kwamba muda mwingi alikuwa akijifungia ndani.

Kwa upande wake, mwanamke huyo, alisema hakuwapo nyumbani hapo wakati tukio la mpenzi wake huyo akijiua.

Alisema aliporejea kutoka nyumbani kwao alikokuwa kwa siku kadhaa alikumbana na mkasa huo wa kukuta mpenzi wake huyo kujiua.

"Nimekuja kutoka nyumbani kijijini nilipofika hapa nilikuta mlango umefungwa, niligonga bila ya mafanikio, nikaondoka kwenda kumuita kaka yake, tukachungulia dirishani tukaona mtu kama amesimama kumbe amejinyonga," alisema.



Baadhi ya mafundi cherehani wa kiwanda cha kuzalisha magodoro cha Family Foam kilichopo Iwambi jijini Mbeya, wakiendelea kushona foronya kwa ajili ya magodoro juzi, wakati wa ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya ilipokagua kiwanda hicho. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kampuni zajitosa kutokomeza utapiamlo

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KAMPUNI za ununuzi wa parachichi zimeahidi kuchangia zaidi ya shilingi milioni 14 kampeni ya kupambana na tatizo la lishe duni na kutokomeza utapiamlo mkoani hapa.

Ahadi hiyo ilitolewa kwenye kikao cha Mkuu wa Mkoa wa Njombe na wadau wa zao la parachichi kilichofanyika ofisini kwake.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Kampuni ya Avo Afrika, Najib Karmal, alisema wameona umuhimu wa kuunga mkono kampeni hiyo ya siku kwa maslahi ya taifa.

"Wadau wote wa parachichi kwa Mkoa wa Njombe wamechangia katika kampeni ya lishe kwa sababu programu hii ni ya Mheshimiwa Rais wa Tanzania (Samia Suluhu Hassan) na tumekubaliana kutoa mchango huu ili kusaidia kampeni hii," alisema Karmal.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, alipongeza jitihada za wafanyabiashara hao na kwamba michango hiyo pamoja na ya wadau wengine itasaidia kuendesha kampeni hiyo katika wilaya zote za mkoa huo.

"Mchango huu ambao umefanya na makampuni ya Ovacado kuunga mkono kampeni ya lishe ni mchango mkubwa na tunaamini mwisho wa kampeni hii tutakuwa tumejenga jamii mpya ya Wananjombe katika eneo zima la siku 1,000 za mjamzito mpaka anapokwenda kujifungua," alisema Mtaka.

Mtaka aliwakumbusha wakazi mkoani hapa wakilima mazao kukumbuka kula mlo kamili badala ya kuuza mazao yao na kuendelea kula chakula cha aina moja.

"Watu wa Njombe wamekuwa na kawaida ya kupika makande Jumatatu, anaendelea kuyapasha kwa wiki nzima kwa hiyo unakuta wiki nzima anaongeza maji na chumvi au mtu anapika viazi mviringo anaviacha nyumbani vinaendelea kupashwa wiki nzima sasa huu sio aina ya ulaji wa chakula," alisema Mtaka.

Mmoja wa wakazi wa Njombe, Richard Ezekiel, alishauri kufanyika kwa tathmini ya kampeni ambazo zimekuwa zikifanyika mara kwa mara ili kupata matokeo chanya na kuondokana na tatizo la utapiamlo.

"Mwisho wa kampeni kuwe na mwendelezo na programu ya ufuatiliaji ili kupata matokeo ya tulichokifanya kimeleta matokeo gani," alisema Ezekiel.



## Watakiwa kuwa kidijitali ukusanyaji takwimu za samaki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIONGOZI wa maeneo ya kuuzia samaki katika wilaya za Unguja wametakiwa kutumia mfumo wa kisasa na kuachana na mfumo wa zamani wakati wa ukusanyaji wa takwimu za samaki katika maeneo ya kazi.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Soud Hamed kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya matumizi ya simu za kisasa huko Maruhubi Wilaya ya Magharibi "A" Unguja.

Dk. Salum alisema mafunzo hayo yanalengo la kuwajengea uwezo watendaji wa maeneo ya kupokelea samaki katika kupata takwimu sahihi za samaki aina ya taa na papa ili kuendana na taarifa ambazo zinazohitajika kuwasilishwa katika Shirika la Chakula Duniani (FAO).

Mkurugenzi huyo alisema kuwa mradi wa heshimu bahari kupitia Taasisi ya Wildlife Conservation Society (WCS) umewapatia wakuu wa maeneo hayo simu saba zenye gharama ya Sh. milioni 2.8 ambazo zitatumika kwa ajili ya uchukuaji wa takwimu za samaki nchini.

Alisema uwepo wa mradi wa heshimu bahari umewasaidia wakuu hao kutumia vifaa ambavyo vitawasaidia kujua takwimu ambazo zinahitajika katika mashirika ya kimataifa ikiwamo FAO na mengine.

Mwakilishi wa Taasisi ya Knowledge Management Lead (heshimu bahari) kutoka USAID, Dk. Salome Shayo, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuwa makini na uchukuaji wa takwimu kutokana na matumizi ya mfumo ambao utasaidia kuendeleza au kutunga mipango sahihi ya uhifadhi wa rasilimali za samaki papa na taa ambao wako hatarini kutoweka Tanzania.

Washiriki wa mafunzo hayo waliishukuru WCS na idara ya maendeleo ya uvuvi na mazao ya baharini kupitia mradi wa heshimu bahari kwa kuwapatia vifaa vya uchukuaji wa takwimu.

# Utafiti: Zanzibar inazalisha taka tani 654 kwa siku

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Mamlaka ya Mazingira, Sheha Mjaja Juma, amesema kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2018 uliofanywa na Benki ya Dunia (WB) Zanzibar inazalisha taka tani 654 kwa siku ambapo kwa mtu mmoja anazalisha taka kilo 0.5.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar wakati akizungumza na Nipashe kuhusu uhifadhi wa taka ambao hatoathiri hali ya kimazingira.

Alisema taka hizo asilimia 80 ni taka zinazooza na asilimia 20 ni taka ngumu zisizooza na miaka ya nyuma taka hizo zikihifadhiwa bila ya kuzingatia taratibu za athari za kimazingira ambapo zikihifadhiwa kwa kuchimbwa shimo.

Alisema kwa sasa teknolojia imekuwa na serikali imeandaa jaa za kitaalamu lililopo huko eneo la Kibele Wilaya ya Kati Unguja ambapo uhifadhi wake umezingatia athari za kimazingira. Juma alisema nia ya serikali ni kuendeleza majaa hayo ya kisasa ya kuhifadhi taka kwa kila mkoa na kushirikiana na sekta binafsi ili zihifadhiwe na kuitumia asilimia 80 ya taka zilizooza kwa ajili ya kutengeneza mbolea na kukuza kilimo.

Alisema zipo kampuni zipatazo 10 visiwani Zanzibar ambazo huchakata taka na kutengenezwa bidhaa zingine na hilo ndiyo lengo la serikali kuhakikisha taka zinazotumika kama bidhaa na siyo uchafu.

"Lengo la serikali ni kuhakikisha taka siyo uchafu bali ni bidhaa, tunaweza kuzitumia katika kuongeza ajira na kuimarisha usafi wetu wa miji," alisema.

Akizungumzia athari za mabadiliko ya tabianchi, Farhat Mbarouk Mkurugenzi Idara ya Mazingira alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2012 maeneo 43 Zanzibar yameathirika na mabadiliko ya tabianchi.



Wananchi wakiangalia sehemu ya jengo lililokuwa ofisi ya Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) jinsi lilivyobomoka juzi Mjimkongwe, Zanzibar. Jengo hilo linafanyiwa matengenezo ya kuwa hoteli. Wafanyakazi 16 wamenusurika, mmoja aliokolewa na kukimbizwa Hospitali ya Mnazi Mmoja. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# TTCL yajivunia mageuzi ya kiuchumi miaka 60 Mapinduzi

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Mawasiliano Tanzania (TTCL) limesema katika kipindi cha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar limeleta mageuzi ya kiuchumi kupitia matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Meneja wa shirika hilo (Zanzibar), Hillary Mwinyi, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonesho ya 10 ya kibiashara yaliyofanyika Uwanja wa Fumba Zanzibar.

Mwinyi alisema TTCL imefanya mambo makubwa ikiwa ni pamoja na kuziunganisha nchi kadhaa ambazo zinapita katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambazo ni Burundi, Malawi, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Katika maonesho hayo TTCL iliweka miundombinu ya mawasiliano na kurahisisha upatikanaji wa huduma maeneo hayo.

Mwinyi alisema katika miaka 60 ya Mapinduzi, shirika hilo limehakikisha mawasiliano yanaimarika ili kuendana na ukuaji na mahitaji ya teknolojia ya mawasiliano na hivyo kuwapa wananchi uwezo wa kuwasiliana kwa kasi na ubora.

Alisema shirika linajivunia kurahisisha zaidi shughuli za kijamii na kiuchumi kutokana na kuviunganisha visiwa vya Pemba na Unguja kwa njia ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

TTCL imetumia fursa ya maonyesho hayo yaliyoandaliwa na Wizara ya Biashara Zanzibar kutoa elimu, kuwapa ufahamu wananchi wanaofika katika banda lao.

# Sekta ya utalii kufanyiwa utafiti ili iwe endelevu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema iko katika mchakato wa kuifanyia utafiti sekta ya utalii kwenye nyanja zote ili iweze kuwa endelevu pasipo kuiathiri jamii, urithi, tamaduni za kizanzibari na mazingira.

Katibu Mkuu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Fatma Mbarouk Khamis, aliyasema hayo jana visiwani hapa alipokuwa akizungumza katika kikao kazi cha wataalamu na wadau wa utalii Zanzibar.

Alisema lengo la utafiti huo ni kutathmini ukomo wa uwezo wa Zanzibar wa kuhimili watalii wanaoingia nchini pasipo kuleta madhara yoyote kwa nchi na wananchi.

Aidha alisema kuwa hatua hiyo itasaidia kufikia malengo ya serikali ya kuweka sekta hiyo kuwa sekta mama ya kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.

Akizungumzia hatua hiyo, mshauri elekezi wa wizara hiyo, Prof. Haji Semboja, alisema kumekuwa na ongezeko la watalii wa ndani na wageni toka nchi mbalimbali duniani, hivyo kufanyika kwa utafiti huo kutasaidia kupata maoni ya wadau, wananchi na wataalamu juu ya namna bora ya kuimarisha huduma na miundombinu.


Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni Africom Limited ambayo ni washauri elekezi wa mradi wa utafiti wa Zanzibar Tourism Carrying Capacity (ZTCC), Kassim Abdi Kassi, alishukuru serikali kwa kuiamini Africom na kuahidi kusimamia vyema mradi huo ili uweze kuleta matokeo chanya na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Kadhalika washiriki wa kikao hicho waliwashauri wataalamu hao kuyatizama kwa kina maeneo ambayo bado hayapo vizuri katika sekta hiyo kwa lengo la kuyaimarisha ili wageni wanapokuja nchini waweze kufurahia vivutio na huduma za kitalii.

Takwimu za mwaka 2023 zinaonesha kuwa zaidi ya watalii 500,000 waliingia nchini na kuchangia asilimia 80 ya pato la fedha za kigeni na asilimia 35 ya wafanyakazi waliajiriwa katika sekta hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**JULIETH BENARD RICHARD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3502-0051 kilichotolewa na OYSTERBAY SECONDARY mwaka 2014. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0138-0516 kilichotolewa na MPWAPWA SECONDARY mwaka 2017. Cheti cha Chuo chenye namba T/UDOM/2017/05081 kilichotolewa na THE UNIVERSITY OF DODOMA mwaka 2021. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/6809/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SIMEO S. DIDAS** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S2213-0586 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **USEVYA SEKONDARI** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/7567/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**THEOPHIL SIMEON NZOYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2768/0404** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ULONGONI SEKONDARI** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/41471/2023.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**HONEST KAROLI TEMU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0372-0070 kilichotolewa na KARUA SECONDARY mwaka 2014. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S1061-0530 kilichotolewa na MAKIBA SECONDARY mwaka 2017. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: KIL/MOS/RB/102743/2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na……02/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: ATHUMANI SALEHE MDOE WA KIHONDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA SIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA MARIAM ATHUMANI MDOE**

## TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 25 Mwezi 01 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**;

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 17 mwezi 01 mwaka 2024**

**HAKIMU MFAWIDHI**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DIANA- GLORY JOACHIM MAKOI**

Anatangaza kupotelewa na cheti cha Kidato cha nne chenye index namba **S0205-0034** kilichotolewa na Baraza la mitihani kupitia **KIBOSHO SECONDARY SCHOOL** Novemba 2014 Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa polisi: **PHQ/ KIL/MOS/1027/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**RAHELI JOHN MOSHA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye namba za usajili MC 216 CBJ aina ya RE New Model, rangi ya BLUE, Chassis No. MD2A25BZ0JWD75163. Engine No. AZZWJD33105. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/138424/2019.**

**THE REGISTRATION OF DOCUMENT CAP 117**
**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**

By the deed poll I AGNESS AWEDI LYATUU (new name) of P.O.BOX-MOSHI. Utterly renounced relinquish and abandon the use of my former name of LILIAN JOSEPH BAKWA (old name )in lieu of and substitution of my former name AGNESS AWEDI LYATUU(new name ). Reason for changing the name is to abandon the name of LILIAN JOSEPH BAKWA (LILIAN has been used to school and JOSEPH BAKWA is a name of my husband) which used to NMB Bank to the name of AGNESS AWEDI LYATUU (AGNESS is a baptism name and AWEDI LYATUU is my father names) which appears to the Citizen Identity Card with number 19470228251170000016.

For the purpose of evidencing such determination, I hereby declare that I shall at all times have after in all records, deeds documents and other writing and in all actions suit and proceeding as well in Public and private dealing and transactions and on all occasion whatsoever use and subscribe the said name AGNESS AWEDI LYATUU (new name) so relinquished as aforesaid but by the name LILIAN JOSEPH BAKWA (older name)

I hereby expressly authorized and require all and ever person whomsoever at all times after the hereof to designate describe and address me by the adopted name AGNESS AWEDI LYATUU (new name) accordingly.

In witness thereof I have set my hand at Moshi
This 24 Day of July 2023
At Moshi.
Signed and delivered by the said
AGNESS AWEDI LYATUU
Who is known to me personally/identified to me
By ……
In my presence this 24 day of July 2023

DEPONENT



BEFORE ME:
Name GLORY JOSEPH TAIRO
Signature ……
Postal address 7749 MOSHI
Qualification ADVOCATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI**
**UHAMIAJI**

## OMBI LA URAIA WA TANZANIA



**Hii ni kwa taarifa kwamba:**
**RAHMA MOHAMED KOMBO**
**S.L.P 20901, DAR ES SALAAM.**

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mhe. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni MKENYA. Nchi atokayo ni KENYA. Shughuli zake ni MAMA WA NYUMBANI na anwani yake ni S.L.P 20901 Dar es salaam. Yupo hapa nchini tangu 2011. Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa kwa maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb Na. DN. 519166.

Kny: KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 279 LA 2023**
**MOHSIN MOHAMEDTAKI ABDALLAH………MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**VIII MINERALS & METALS TANZANIA LIMITED…MDAIWA**

## WITO KUITWA SHAURINI

**VIII MINERALS & METALS TANZANIA LIMITED – POPOTE ULIPO/MLIPO**

MOHSIN MOHAMEDTAKI ABDALLAH amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 06/02/2024 saa 3:00 asubuhi mbele ya Mh. J.W. SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 09 Mwezi 01, 2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTE KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI. TUPIGIE: +255 - 0677020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Bunge lapitisha muswada tata wahamiaji kuhamishiwa Rwanda

**LONDON,** Uingereza

BUNGE la Uingereza limepitisha muswada wenye utata unaotoa ruhusa ya watu wanaoingia nchini humo kuomba hifadhi kuwapelekwa nchini Rwanda.

Hata hivyo, mswada huo umeibua mpasuko katika Chama cha Conservative na baadhi ya viongozi wake wamejiuzulu.

Wabunge 320 walipiga kura ya kukubali na 276 walipiga kura ya hapana.

Siku moja kabla ya upigaji kura, wabunge 60 wa chama tawala kinachoongozwa na Waziri Mkuu Rishi Sunak walitangaza kuupigia kura ya hapana mswada huo.

Mzozo huo ulisababisha pia manaibu wawili wa chama chake cha kihafidhina kujiuzulu na kutangaza kupinga mpango huo.

Lakini wakati wa upigaji kura bungeni, ni wabunge 11 pekee wa chama hicho waliopinga mswada huo. **RFI**



# Hali tete mashariki ya kati, mapigano yaanza kuenea

**KARACHI,** Pakistan

HALI imekuwa tete katika ukanda wa mashariki ya kati baada ya nchi za Iran na Pakistan kutunishiana misuli kwa kushambuliana kwa makombora.

Jana Pakistan ilisema imefanya mashambulizi ya makombora eneo la Iran, siku tatu baada ya shambulio kama hilo kutekelezwa na Iran ikidai kulenga kambi za magaidi.

Katika taarifa yake, Pakistan ilisema imefanya mashambulizi hayo kwa lengo la kuyapiga maficho ya magaidi katika eneo la mpakani la Sistan-o-Balochistan. Hata hivyo, vyombo vya habari vya Iran viliripoti kuwa wanawake watatu na watoto wanne wameuawa katika tukio hilo.

Nchi hizo mbili zimekuwa zikilaumiana kwa muda mrefu kwa kuhifadhi makundi ya wapiganaji wanaofanya mashambulizi katika maeneo ya mpaka wa pande zote.

Jumatano jioni, vyombo vya habari vya Iran viliripoti kwamba milipuko kadhaa ilisikika karibu na mpaka wake na Pakistan, karibu na mji wa Saravan.

Aidha, Wizara ya Mambo ya Nje ya Pakistan ilithibitisha mashambulizi hayo katika taarifa yake, na kueleza idadi isiyojulikana ya magaidi waliuawa wakati wa operesheni hiyo ya kijasusi.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya nchi hiyo kulaani vikali shambulizi lililofanywa na Iran Jumanne, ambalo liliuawa watoto wawili.

Kwa upande wake Iran ilisema mashambulizi hayo yalilenga kundi la waasi lenye makao yake Pakistan, lakini Pakistan ilisema raia waliuawa.

Baada ya tukio hilo Pakistani iliahidi kulipiza kisasi na ilimzuia balozi wa Iran kurejea nchini humo na pia ilimtimua mjumbe wake.

Iran ilisisitiza kuwa mashambulizi yake yalilenga kundi la Jaish al-Adl, ambalo lilitaja kuwa la kigaidi na kukana kuwaua raia.

Wakati huo huo, Marekani ilisema imetekeleza shambulio la nne dhidi ya wanamgambo wa Wahouthi wanaotawala nchi ya Yemen.

Wizara ya Ulinzi ya Marekani ilisema hatua hiyo inatokana na urushwaji wa makombora 14 kutoka Yemen dhidi ya meli zinazokatisha Bahari ya Shamu.

Taarifa kutoka kamandi ya jeshi ya mashariki ya kati, ilisema maeneo hayo yalipigwa na makombora ya Tomahawk yaliyorushwa kutoka kwenye meli za Marekani.

Mshauri wa Usalama wa Kitaifa wa Marekani, Jake Sullivan, alisema hatua hiyo ni kujibu mashambulizi yanayoendelea ya wanamgambo hao dhidi ya meli za kibiashara katika eneo hilo.

Waasi wa Houthi walianza kushambulia meli za wafanyabiashara mwezi Novemba, wakisema walikuwa wakilipiza kisasi kutokana na operesheni ya kijeshi ya Israel katika Ukanda wa Gaza.

Tangu wakati huo, kundi hilo limeanzisha mashambulizi kadhaa dhidi ya meli za kibiashara zinazopitia Bahari ya Shamu, moja ya njia yenye shughuli nyingi zaidi duniani.

Hivi karibuni kundi hilo lilisema liliipiga meli ya Genco Picardy kwa makombora na kusababisha Marekani kuanza kushambulia kwa makombora maeneo mbalimbali ya Yemen. **BBC**




Waandamanaji wa vuguvugu la Wakit Tamma nchini Chad wakiweka kuzuizi cha gari la matangazo katika barabara kuu wakishinikiza Rais Jenerali Mahamat Idriss Deby kuondoka madarakani jana. **PICHA: AFP**

# Mfalme, binti mfalme wa Uingereza wagonjwa

**LONDON,** Uingereza

MFALME wa Uingereza, Charles III, ametangazwa kuwa ana ugonjwa wa tezi dume na anatarajiwa kufanyiwa upasuaji wiki ijayo.

Katika taarifa iliyotolewa na kasri la kifalme la Kensington, ilieleza pia binti mfalme wa Wales, Kate Middleton, anaendelea kupata nafuu baada ya kulazwa hospitalini kutokana na kufanyiwa upasuaji.

Taarifa hiyo ambayo iliwashtua raia wengi wa nchi hiyo, ilisema Kate atajiuzulu wadhifa wake wa kifalme kwa miezi kadhaa baada ya upasuaji huo wa ugonjwa usiowekwa wazi kufanikiwa.

Matangazo kuhusu afya za wanafamilia ya kifalme zilitolewa ndani ya saa mbili nyakati ya Alasiri ya Jumatano.

Taarifa kuhusu afya za wanaufalme kwa kawaida huwa ni siri inayolindwa sana na hutangazwa kwa umma kwa maelezo machache.

Baada ya kutolewa kwa taarifa hizo mbili, watu wengi walionekana kushtushwa na kushangazwa.

Taarifa ya kwanza ilitolewa saa nane za alasiri na kasri la Kensington ikifichua kwamba binti mfalme Kate amelazwa katika hospitali ya kibinafsi katikati mwa jiji la London, Jumanne kwa ajili ya kupatiwa matibabu.



Mfalme Charles III wa Uingereza na binti Mfalme Kate.

Ilieleza afya ya mwanamfalme huyo ambaye anatarajia kuwa malkia baada ya mume wake William kurithi kiti hicho inaendelea vizuri.

Inafahamika kwamba anaendelea vizuri, lakini anatarajiwa kukaa hadi wiki mbili hospitalini hadi baada ya Pasaka huku akiendelea kupata nafuu kwa muda wa miezi kadhaa.

Wote wawili hawakuwa na dalili ya kuumwa wakati walipoonekana pamoja Sandringham wakati wa sikukuu ya Krismasi.

Dakika 90 baadaye, taarifa ilichapishwa na kasri la Buckingham ikieleza Mfalme Charles III, anahitaji matibabu ya kurekebisha tezi dume wiki ijayo.

Matatizo hayo ni ya kawaida kwa wanaume wenye umri mkubwa sio saratani. Mfalme alitimiza miaka 75 mnamo Novemba mwaka jana.

Haijulikani ni upasuaji gani atakaofanyiwa mfalme hiyo, lakini taarifa hiyo atapata nafuu muda mfupi baada ya matibabu.

Katika hali kama hiyo washauri wa serikali wanaweza kufanya kazi kama wasimamizi wa mfalme na kutekeleza majukumu kama vile kusaini hati rasmi. **BBC**

HABARI MICHEZO

# AZAM FC YATAMBIA USAJILI WAKE, KUWEKA KAMBI Z'BAR

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Azam FC umesema usajili wa maboresho walioufanya kipindi cha dirisha dogo utawasaidia katika kuimarisha timu hiyo kwenye michezo ya Ligi Kuu na komba la FA.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Thabit Zakaria 'Zaka' amesema usajili wao huo ni wa maboresho na umezingatia mahitaji ya timu hiyo.**

Aidha, alisema uongozi wa timu hiyo umeamua kuipeleka Zanzibar kwa ajili ya kuweka kambi kujiandaa na michezo ya Ligi Kuu baada ya kurejea Dar es Salaam hivi karibuni wakitokea visiwani humo walipokwenda kwa ajili ya michuano ya Kombe la Mapinduzi.

"Baada ya usajili wetu wa maboresho, tunatarajia kurudi Zanzibar kuweka kambi, itawasaidia makocha wetu kukaa na wachezaji wapya na kutengeneza muunganiko wa timu yetu," alisema Zaka.

Zaka alisema kambi hiyo itaanza rasmi Januari 25, baada ya siku mbili za wachezaji kuanza mazoezi.

"Tulipomaliza Kombe la Mapinduzi tuliwapa mapumziko wachezaji wetu hadi tarehe 23 watakapoanza mazoezi, halafu tarehe 25 tutakwenda kuweka kambi kwa ajili ya kufanya maandalizi yetu kwa ajili ya michezo ya Ligi Kuu na Kombe la FA," alisema Zaka na kuongeza,


"Labda watu watajiuliza kwa nini Zanzibar? Ni sehemu nzuri ambayo itatupa utulivu wa kutosha kwa ajili ya wachezaji kuwa makini na kupokea kile ambacho wanajiandaa nacho, kwa sasa kuna viwanja vizuri na mazingira mazuri pia, hoteli kama kawaida huwa ni nzuri na hakuna vurugu nyingi, vile vile hali ya hewa ni kama Dar es Salaam tu," alisema Zaka.

Akizungumzia usajili, alisema wanaamini wamesajili wachezaji wazuri ambao watakuja kuongeza ubora kwenye kikosi.

"Tunatarajia wachezaji bora watuongezee ubora kwenye timu yetu, tunajua kikosi chetu msimu huu ni bora, lakini siku zote ubora huwa hauna mwisho, tunaamini uzoefu, maarifa na jitihada zao zinaweza kutusaidia," alisema.

Azam imewasajili wachezaji Franklin Navaro kutoka Tulua FC ya Colombia, Yeison Fuentes kutoka Itagui FC pia ya Colombia na Mohamed Mustafa kutoka El Merrikh ya Sudan ambaye yupo kwa mkopo wa miezi sita.

Azam wanaongoza ligi kwa sasa wakiwa na pointi 31 baada ya kucheza michezo 13 na kufanikiwa kushinda michezo 10, kutoka sare mchezo mmoja na kupoteza mchezo mmoja.




Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, Linah Shayo, akipokea mfano wa hundi ya Shilingi milioni tano jana kutoka kwa Meneja wa Tigo Kanda ya Temeke na Kigamboni, Jansen Msechu, baada ya kuibuka mshindi wa promosheni ya magifti dabodabo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkazi Dar ashinda magifti dabodabo

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Dar es Salaam, Linah Shayo, jana alitangazwa kuwa mshindi wa zawadi ya shilingi milioni tano katika promosheni ya magifti dabodabo inayoendeshwa na kampuni ya huduma za simu ya Tigo.

Lina anayeishi Kigamboni, ameibuka mshindi kwenye droo ya wiki iliyopita na kukabidhiwa zawadi yake na Meneja wa kampuni hiyo kanda ya Temeke na Kigamboni, Jansen Msechu.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa zawadi hiyo, Linah alisema hakuamini pale alipopigiwa simu na mfanyakazi wa kampuni hiyo kumpa taarifa ya ushindi huo.

"mimi naishi kata ya Kibugomo, wilaya ya Kigamboni, kwa kweli nina furaha sana, nawashukuru Tigo kwa kuwa wa kweli katika promosheni zao, nimekuwa mtumiaji wa line ya Tigo kwa miaka mingi, pesa hizi zitanisaidia sana, nawashukuru kwa kweli," alisema Linah.

Aidha, alisema ushindi huo umetokana na kutumia huduma za Tigo hasa Tigopesa kwa kufanya miamala mbalimbali kila wakati na kupata nafasi ya kushinda.

"Nimekuwa nikifanya miamala ya kununua vitu au kununua muda wa maongezi kwa kutumia Tigopesa, nawashauri na wengine wafanye hivi wanaweza wakaibuka washindi," alisema Linah.

Akizungumza wakati wa kumkabidhi zawadi hiyo, Msechu, alisema kwa mara ya kwanza mkazi wa Kigamboni ameibuka mshindi wa promosheni hiyo na kuwataka wateja wengine kuendelea kufanya miamala kuweza kupata nafasi ya kuibuka washindi.

Alisema promosheni hiyo inaendelea na wanatarajia kutoa zawadi kubwa ya gari mpya na pesa shilingi milioni 30 mwishoni mwa promosheni hiyo.

" Kwa sasa tunaendelea kutoa zawadi ya pesa kuanzia milioni moja mpaka milioni 10, lakini pia vifaa vya umeme vya majumbani, wateja waendelee kuchangamkia fursa hii," alisema Msechu.

## KVZ yajipanga, inautaka ubingwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya maafande wa KVZ imepania kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar na sasa inajipanga kwa ajili ya mzunguko wa pili wa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ali Mohamed, alisema katika kipindi hiki wanachosubiri mzunguko wa pili wa ligi hiyo ameendelea kuiimarisha timu yake kwa mbinu mbalimbali mazoezini.

Alisema mazoezi yake yanalenga kuondoa mapungufu na kasoro alizoziona kwenye timu hiyo wakati wakishiriki michuano hiyo ya Mapinduzi iliyomalizika hivi karibuni na kushuhudia Mlandege wakitwaa ubingwa kwa mara ya pili mfululizo. Alisema kikubwa anachokihitaji katika kikosi hicho hivi sasa ni kupata muunganiko mzuri baina ya wachezaji wapya waliowasajili katika dirisha dogo pamoja na wale wa zamani.

Aidha alisema katika kuhakikisha mpangilio huo wa mazoezi unafanikiwa wamejipangia kucheza michezo mingi ya kirafiki kabla ya kurejea kwenye ligi.

Alisema wamepanga kucheza michezo mitatu ya kirafiki na timu za daraja la kwanza na ligi za mikoa.

## Timu ya Taifa wenye Ulemavu kuingia kambini

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha wachezaji 20 wa Timu ya Taifa ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu kinatarajia kuanza kambi ya nje wiki ijayo kwenye uwanja wa Uhuru Dar es Salaam kujiandaa na mashindano ya Afrika yatakayoanza Aprill 19 Cairo, nchini Misri.

Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa watu wenye ulemavu Tanzania (TAFS), Vincent Kaduma, amesema miongoni mwa wachezaji hao mchezaji mmoja anatoka Arusha, watatu wanatoka Zanzibar na wachezaji 16 wanatoka Dar es Salaam.

Alisema lengo la mashindano hayo ni kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwaka 2026 baada ya nchi kutangazwa. Rais huyo alisema maandalizi yanaendelea vema na muda wowote kuanzia sasa watatangaza timu watakazocheza nazo michezo ya kirafiki.

Aidha alisema anaishukuru serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kwa kuhakikisha timu hiyo inaanza kambi ya nje na muda mfupi ujao wataanza kambi ya ndani.

## ZISIKUPITE

### PHILLIPS AGOMBEWA ULAYA

ATLETICO Madrid na Barcelona ni kati ya klabu sita zinazowania kumsajili kiungo wa kati wa England, Kalvin Phillips, kutoka Manchester City, huku mustakabali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 ukitarajiwa kuamuliwa wiki ijayo. ***(Telegraph)***

### SPURS YAMFUATA GALLAGHER

KLABU ya Tottenham Hotspur haijakata tamaa ya kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 23 kutoka Chelsea. ***(Football Insider)***

### BROJA NJIA MOJA

CHELSEA iko tayari kumruhusu mshambuliaji wa Albania, Armando Broja, mwenye umri wa miaka 22 kuondoka kwa mkataba wa kudumu iwapo ofa inayofaa itapokelewa, huku West Ham, Fulham na Wolves zikiwa miongoni mwa klabu zinazomwania. ***(Mail)***

### RAMOS MAMBO MAGUMU

MUSTAKABALI wa mshambuliaji wa Ureno, Goncalo Ramos, katika klabu ya Paris St-Germain uko mashakani na vigogo hao wa Ufaransa wanaweza kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 Januari hii iwapo ofa inayofaa itatolewa. ***(L'Equipe)***

### CHOLABAH ANUKIA FULHAM

FULHAM ipo katika mazungumzo ya kumsajili beki wa kati wa Chelsea, Trevoh Chalobah, 24, kwa mkataba wa mkopo wa miezi sita na chaguo la kumnunua. ***(Florian Plettenberg kwa Sky Germany)***

### HOJBJERG ATAJWA NAPOLI

NAPOLI itavutiwa na kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 28, ikiwa Tottenham Hotspur itaamua kumuuza mchezaji huyo Januari hii. ***(Telegraph)***

### SIMONS AKARIBIA ARSENAL

ARSENAL inaongoza kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Uholanzi, Xavi Simons, mwenye umri wa miaka 20, ambaye yuko kwa mkopo RB Leipzig kutoka Paris St-Germain. ***(Sport Bild)***

### BRUNO ANUKIA ARSENAL

ARSENAL pia wamepewa nguvu katika kumsaka kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes, 26, kufuatia ripoti ya Newcastle United inatafuta mbadala wake. ***(Football London)***

### REYNA ATAJWA VILLA

KLABU ya Aston Villa imeulizia kwa Borussia Dortmund kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Marekani, Giovanni Reyna, 21. ***(Football Transfers)***

### BENRAHMA SOKONI TENA

KLABU ya Marseille inapanga kurejea kutoa ofa kwa winga wa West Ham, Said Benrahma, baada ya ofa ya kwanza kwa mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Algeria mwenye umri wa miaka 28 kukataliwa. ***(Foot Mercato)***

## DONDO SOKA
## MAGAZE ULAYA




# BENZEMA APANGA KUTIMKA SAUDIA

**Inaelezwa nyota huyo ana nafasi kubwa ya kurejea England...**

**RIYADH,** Saudi Arabia

KARIM Benzema anafikiria chaguzi ya mahali gani atakwenda kwenye dirisha la usajili la Januari hii baada ya miezi sita ya kukaa na klabu ya Ligi Kuu Saudi Arabia, Al Ittihad, kwa mujibu wa ESPN.

**Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 36 hajafurahishwa na jinsi kibarua chake nchini Saudi Arabia kinavyozidi kuimarika hadi sasa, licha ya mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or 2022 kufunga mabao 15 katika michezo 24 ya michuano yote tangu ajiunge na ligi hiyo akiwa mchezaji huru.**

Klabu hiyo inasemekana haitaki kumruhusu mchezaji huyo kuondoka kwa mkopo au kwa mkataba wa kudumu.

Hata hivyo, mchezaji mwenzake kwenye klabu hiyo, Jordan Henderson, amesimama kama mfano wa mchezaji ambaye amefanikiwa kufanya mazungumzo ya kuachiwa kutoka kwenye mkataba wake na Al Ettifaq. Al Ittihad wametatizika msimu huu na wako nafasi ya saba katika msimamo wa ligi wakiwa na pointi 25 nyuma ya viongozi Al Hilal walioshinda taji msimu uliopita.

Benzema, ambaye amebakiza miaka miwili na nusu katika mkataba wake, amekosolewa na vyombo vya habari vya Saudia Arabia kwa uchezaji wake.

Vyanzo vimeiambia ESPN Ligi Kuu England inaweza kuwa chaguo kwa Benzema, na klabu nyingi pamoja na Chelsea, vinaonyesha nia ya kumnunua mshambuliaji huyo mkongwe.

Kurejea Real Madrid, ambako mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Ufaransa alikaa kwa miaka 14, hakusemwi jambo linalowezekana.

Benzema bado amekwama nchini Mauritius baada ya kimbunga cha kitropiki cha Belal kupiga eneo hilo na kusimamisha safari zote za ndege zinazoingia na kutoka kisiwani humo.

Al Ittihad wako katika kambi ya mazoezi Dubai, na Benzema atajiunga na kikosi na Kocha Marcelo Gallardo, mara tu atakapoweza.

Mapema wiki hii, Benzema aliwasilisha kesi ya kudhalilishwa mahakamani akimshtaki Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ufaransa, Gérald Darmanin, ambaye alimshutumu nyota huyo kuwa na uhusiano na Kundi la Muslim Brotherhood.

# ONANA KAMILI KUITUMIKIA CAMEROON KATIKA AFCON




**ABIDJAN,** Ivory Coast

GOLIKIPA wa Manchester United, André Onana, huenda akajumuishwa katika kikosi cha Cameroon kwa ajili ya mechi ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), dhidi ya mabingwa watetezi, Senegal itakayochezwa leo baada ya kurejea mazoezini na timu hiyo hapo juzi.

Onana alikosa mechi ya ufunguzi ya michuano hiyo inayofanyika Ivory Coast baada ya kuruhusiwa kusalia Manchester United na kucheza katika sare ya 2-2 dhidi ya Tottenham Hotspur Jumapili iliyopita.


Alisafiri kwa ndege ya kukodi usiku kucha hadi Ivory Coast baada ya mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Old Trafford, lakini alifika saa chache tu kabla ya kuanza kwa mpambano wa Kundi C dhidi ya Guinea, ambapo Cameroon walitoka nyuma na kulazimisha sare ya 1-1.

Uamuzi wa kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kuacha mechi ya ufunguzi wa michuano hiyo ilizua utata miongoni mwa mashabiki wa Cameroon.

Katika mahojiano baada ya kuwasili Ivory Coast, Onana aliwaambia waandishi wa habari juu ya mvutano mgumu wa uaminifu kati ya klabu na nchi, haswa kwa wachezaji wa kimataifa wa kutoka Afrika waliolazimika kuziacha klabu zao za Ulaya katikati ya msimu ili kushiriki Fainali za AFCON.

"Ni sawa na kuchagua kati ya baba na mama yangu, lakini nchi yangu inatangulia, ndiyo maana nipo hapa," alisema.

## Ajax yakaribia kumnasa Henderson



**AMSTERDAM,** Uholanzi

AJAX wapo katika mazungumzo ya mwisho kumsajili, Jordan Henderson, baada ya kiungo huyo kufikia makubaliano ya kuondoka Al Ettifaq, kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 anataka kuondoka Saudi Arabia baada ya chini ya miezi sita na amekuwa kwenye majadiliano ya kumaliza mkataba wake mnono mapema.

Chanzo hicho kilithibitisha Henderson sasa amekubaliwa kuachiwa, lakini masharti kamili hayako wazi.

Henderson atachukua punguzo kubwa la mshahara wake kutoka Saudia, inayodhaniwa kuwa angalau pauni 350,000 kwa wiki iwapo atajiunga na Ajax.

Klabu ya Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, imepata makubaliano kimsingi na Henderson na uchunguzi wa kimatibabu unapangwa mjini Amsterdam baadaye wiki hii huku mazungumzo ya mwisho ya mkataba wake yakiendelea.

Vyanzo vya habari nchini Uholanzi vinasema Henderson anaweza kusaini mkataba wa miezi 18 na chaguo la mwaka mmoja zaidi.

Muda mfupi wa Henderson nchini Saudi Arabia umetajwa haukuwa na furaha kwake.

Al Ettifaq wamo katika nafasi ya nane kwenye Ligi ya Saudia Pro League huku Kocha Steven Gerrard, akiwa chini ya shinikizo baada ya msururu wa matokeo mabaya.

## Toney ataka kuchezea klabu kubwa EPL

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Brentford, Ivan Toney, amesema anapanga kuchezea "klabu bora inayoshindania mataji," na hajakata tamaa kuondoka katika klabu hiyo ya London Magharibi mwezi huu kutokana na kuhusishwa na uhamisho wa kutua Chelsea na Arsenal.

Katika mahojiano na Sky Sports, Toney pia alisema analenga kujumuishwa kwenye kikosi cha England kinachonolewa na Gareth Southgate kwa ajili ya michuano ya Ulaya msimu huu baada ya kumaliza adhabu ya kufungiwa kwa miezi nane kwa kukiuka kanuni za kamari za FA.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye mechi yake ya mwisho katika kikosi cha kwanza cha Brentford ilikuwa dhidi ya Liverpool mnamo Mei 6, mwaka jana, ameruhusiwa kufanya mazoezi na wachezaji wenzake tangu Septemba na alifunga hat-trick katika mechi ya kirafiki Southampton uliochezwa Januari 6, mwaka huu.


"Huwezi kamwe kutabiri ni wakati gani mwafaka wa kuhamia kwingine, lakini nadhani ni dhahiri nataka kuchezea klabu kubwa," alisema.

"Kila mtu anataka kuchezea klabu kubwa, ambayo inapigania mataji, inaweza kuwa Januari hii au baadaye kwa klabu kuingia na kulipa fedha zinazofaa, nani anajua?

"Lakini lengo langu kuu ni kufanya kile ninachopenda kufanya uwanjani."

Toney alitambuliwa kama mraibu wa kamari baada ya kukubali ukiukaji wa sheria ya FA kuhusu kamari.

Alipoulizwa inakuwaje katika mtego wa uraibu, Toney alisema: "Nisingeweza kukuambia labda kama vile waraibu wengine. Wakati mwingine, hutambui unachofanya kwa sasa. Wewe tambua tu baadaye unafanya kitu ambacho hupaswi kufanya."



## Mkomweke ashinda Twende Zetu Ki-VIP

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Newala mkoani Mtwara, Haruni Mkomweke, ameingia katika orodha ya washindi wa Kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP ambayo inaratibiwa na Tigopesa kwa kushirikiana na Betika, imeelezwa.

Juzi washindi wawili waliishuhudia mubashara mechi ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), kati ya Timu ya Taifa (Taifa Stars), ilipovaana na Morocco ambayo ilimalizika kwa Tanzania kufungwa mabao 3-0.

Wadau wengine wanne wataishuhudia Stars ikicheza dhidi ya Zambia (Chipolopolo), mechi itakayochezwa keshokutwa, katika fainali hizo zinazofanyika Ivory Coast.

Kaimu Meneja wa Tigo tawi la Newala, Deogratius Tossi alisema, mshindi huyo aliyekabidhiwa runinga ya nchi 70, dishi na dekoda yenye kifurushi ni miongoni mwa washindi kwenye kampeni hiyo.

"Kampeni hii ni rahisi, wateja wanabashiri na Betika kupitia akaunti zao za Tigopesa," alisema.

Awali Ofisa Habari wa Betika, Juvelinaus Rugambwa, alisema katika droo kubwa, tayari washindi sita wa kwenda Ivory Coast wamepatikana.

"Watakwenda Ivory Coast kwa makundi mawili, kundi la kwanza lilishuhudia mechi ya Stars dhidi ya Morocco (juzi) na kundi la pili watashuhudia mchezo wetu na Zambia," alisema na kuwataja baadhi ya waliopata fursa hiyo kuwa ni Nasibu Stanford na Elias Simba.

Katika droo ndogo iliyopita, mashabiki walioshinda runinga ni Edson Musingi wa Morogoro na Bakari Kitenge wa Dar es Salaam.

# SIMBA TAYARI KUPITISHA KATIBA MPYA JUMAPILI

**Na Saada Akida**

KLABU ya Simba imetangaza inatarajia kufanya mkutano mkuu kwa ajili ya marekebisho ya katiba utakaofanyika keshokutwa jijini Dar es Salaam, imeelezwa.

**Mkutano huo wa marekebisho ya katiba unafanyika baada ya kupata maelekezo kutoka katika Baraza la Michezo Taifa (BMT).**

Imepita miaka sita tangu Simba ilipopitisha marekebisho ya katiba kwa ajili ya kubadili muundo wa umiliki na uongozi lakini ilikutana na vikwazo mbalimbali vya kanuni za sheria ya umiliki wa kampuni kilichopelekea Tume ya Ushindani (FCC) kuzuia kwa muda kuendelea kwa mchakato.

Akizungumza jijini jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Hussein Kitta, alisema walikutana na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, kujadili kuhusu mchakato wa mabadiliko ya katiba ya klabu yao na mambo sita yaliainishwa ili kufanyiwa kazi.

Kitta alisema tayari vipengele hivyo mamlaka ya uteuzi wa bodi ya wadhamini baada ya kuteuliwa sasa wajumbe wake wanatakiwa kuchaguliwa katika mkutano mkuu, kuweka wazi nafasi ya kupatikana kwa mwenyekiti, malengo ya katiba na kuweka wazi malengo ya mkutano.

"Lengo ni kukamilisha mabadiliko na serikali ilitupa muda ili kukamilisha jambo hili. BMT walisema kabla ya kupeleka kwa wanachama mlete hiyo rasimu tupitie kwanza. Baada ya vikao tukaenda BMT na nina furaha kuwaambia tumepokea barua kutoka kwao ya kuridhishwa na yale tuliyopitisha," alisema Kitta.

Aliongeza mambo sita yaliyopitishwa yana faida zaidi kwa mwanachama wa Simba kuliko kwa mtu mwingine yeyote na ni kuelekea katika kukamilisha mabadiliko ya uendeshaji.

"Ni wazi mabadiliko yatakwenda kutokea, jambo hilo tutawaachia CEO na bodi. Kazi yangu ni kuratibu maboresho ya vifungu, Katiba inataka wanachama kupata rasimu siku saba kabla ya mkutano mkuu na tayari tumeshawatumia.

Ushirikishwaji wa wanachama ulikuwapo na hata kamati ina wanachama ambao ni wenyeviti wa matawi lakini pia wito wa kuwataka wanachama kutoa maoni ulitolewa kupitia mitandao ya Simba," Kitta aliongeza.




Mshindi wa wiki ya tano wa Kampeni ya Twende Zetu Ivory Coast Ki-VIP, Haruni Mkomweke (katikati), akiwa ameshika runinga aliyokabidhiwa na Meneja wa Tigo wa Tawi la Newala, Deogratius Tossi (kulia). Kushoto ni Kaimu Balozi wa Betika, Haji Balou. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GAMONDI AFUATA MAKALI UFUKWENI

INATOKA UK. 24

watakuwa wapo juu sana kifiziki, wasiachane sana," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema anataka kuona Yanga inaendelea kusaka ushindi katika kila mechi watakayocheza ili kufikia malengo na watafikia hapo kama kila mchezaji atakuwa fiti kimwili na kiakili.

"Tutaendelea hivi hadi nione wamerejea angalau kidogo kwenye utimamu wa mwili ndiyo niangalie suala la kuwapeleka uwanjani, hii inatokana na kuwa na baadhi ya wachezaji wapya ili nao walingane na wenzao, wajue wanacheza vipi na wao waanze kufanya nini ili kutengeneza muunganiko," alisema Gamondi.

Naye Mzize amewataka wapinzani wao kujipanga kupokea vichapo kwa sababu anaamini watarejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na nguvu mara mbili ya ile waliyoonyesha katika mechi zilizopita.

Mzize alisema kusajiliwa kwa baadhi ya wachezaji wapya katika dirisha dogo kutaongeza morali ndani ya kikosi hicho na kila mmoja atajituma ili kujihakikishia namba.

Alisema hakuna mchezaji atakayebweteka kutokana na kila mmoja kuhitaji kucheza na anaamini jambo hilo litaongeza ushindani na kumpa kocha wigo mpana wa kupanga kikosi kizuri katika kila mechi.

"Tunaendelea na mazoezi vizuri ili kujiweka fiti baada ya muda mrefu wa kupumzika kucheza mechi, kila mchezaji anaonekana kufurahia mazoezi.

Naamini ligi ikirudi na mashindano mengine tutakuja kivingine kabisa tofauti na mechi zilizopita, yaani tutakuwa na nguvu mara mbili zaidi, tunataka kutimiza malengo yetu ya kutwaa ubingwa," alisema Mzize na kuongeza;

"Kukiwa na ushindani na ari ya timu inakuwa kubwa kwani kila mchezaji atajituma kupambania namba hivyo morali inaongezeka kikosini," Mzize alisema.

Hadi ligi inasimama Desemba mwaka jana kupisha kambi ya Taifa Stars inayoshiriki AFCON, Yanga iko nafasi ya pili ikiwa na pointi 30 nyuma ya vinara Azam FC wenye pointi 31 lakini wakiwa na michezo miwili zaidi.

## 'Stars tutasonga mbele'

INATOKA UK. 24

yafanyia kazi.

„Tumepoteza, lakini tuna michezo miwili mbele yetu, mimi naamini timu yetu ni nzuri na katika michuano hii tutafika mbali, pamoja na mechi zilizobaki ni ngumu lakini kuna mabadiliko ya kiuchezaji ambayo tutayafanya," Msuva alisema.

Katika hatua nyingine, Miroshi, alilia na Mahamat na kusema alimwonyesha kadi hiyo kimakosa.

„Kuhusu kadi nyekundu kusema kweli sikumgusa kabisa, sasa sijui refa alikuwa anafikiria nini wakati kuna VAR, alilalamika mchezaji hiyo.

Stars itashuka tena uwanjani keshokutwa kuanzia saa 2:00 usiku kucheza dhidi ya Zambia ambayo juzi ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya DRC.



Ajax yakaribia kumnasa Henderson UKURASA 22



Beki wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Ibrahim Hamad (kulia), akiwania mpira dhidi ya Ghanem Saiss wa Morocco katika mechi ya Kundi F ya Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Laurent Pokou mjini San Pedro, Ivory Coast juzi usiku. Stars ilifungwa mabao 3-0. **PICHA: TFF**

# GAMONDI AFUATA MAKALI UFUKWENI

## ●●● Ni kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake, Mzize afunguka...

**Adam Fungamwango na Oliver Albert**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, akiwapeleka wachezaji wake kwenye ufukwe wa Coco kwa ajili ya kufanya mazoezi ya kuwarejesha utimamu wa mwili, mshambuliaji wa timu hiyo, Clement Mzize, ametamba kikosi chao kitarejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara kikiwa 'moto' zaidi.

**Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara wamerejea kuanza programu hiyo ya kwanza ya kuimarisha mwili baada ya kumaliza mapumziko maalumu waliyopewa hivi karibuni baada ya kutoka kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi huko Zanzibar.**

Kikosi hicho kilianza rasmi mazoezi yake juzi kikiwashirikisha wachezaji wote ambao hawako kwenye timu za taifa zinazocheza Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) huko nchini Ivory Coast.

Nipashe iliwashuhudia wachezaji hao wakianza mazoezi ya kukimbia katika mchanga, wakipiga raundi kadhaa, baadaye wakatakiwa kukimbia lakini kwenye maeneo maalum yaliyowekewa kigingi na vikwazo wakitakiwa kuzunguka, kuruka na kuendelea na mwendo.

Halafu nyota hao walitakiwa kukimbia kwa kasi kwenda na kurudi, zoezi ambalo lilikuwa gumzo na burudani kwa mashabiki waliofika kuwatazama.

Baada ya zoezi hilo, wachezaji hao waliingia ndani ya kamba moja, mmoja akiishika na mwingine akiwa ameizungusha kiunoni akiruka huku na huko ili kutengeneza stamina.

Akizungumza na Nipashe, Gamondi alisema ameanza na mazoezi ya aina hiyo kwa sababu anataka awatafutie wachezaji wake utimamu wa mwili kabla ya kuanza kuwapa mbinu nyingine.

"Hii ni mipango yetu, kuna wachezaji walikuwa katika Kombe la Mapinduzi, tukawapa mapunziko mafupi, lakini kuna wengine hawakuwapo kabisa, hawa wote ni lazima waanze mazoezi ya nguvu kwa sababu wenzao kwenye michuano ya AFCON, tunataka wawe sawa, wale wakirudi

INAENDELEA UK. 23

# Amrouche: Stars tutasonga mbele

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya kufungwa na Morocco katika mechi ya kwanza ya Kundi F katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Adel Amrouche, amesema bado ana matumaini ya kusonga mbele katika michuano hiyo endapo watarekebisha makosa yaliyojitokeza hapo juzi.

Stars ilianza kwa kipigo cha mabao 3-0, katika mechi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa San Pedro nchini Ivory Coast, Amrouche amesema kwa asilimia kubwa kadi nyekundu aliyoopewa mchezaji wake, Dismas Miroshi, iliwamaliza.

Amrouche alisema kadi nyekundu aliyoonyeshwa mchezaji wake na mwamuzi, Alhadi Allaou Mahamat, haikupaswa kwa sababu hakumgusa mchezaji wa Morocco.

„Tunakwenda kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwa ajili ya mechi zinazofuata, ikumbukwe bado tuna wachezaji wachanga katika michuano hii, na hiyo ndiyo faida kwao kwa ajili ya kupata uzoefu wa siku za baadaye ambapo inaonekana tutakuwa na kikosi kizuri zaidi.

Tumepoteza, lakini tunakwenda kucheza mechi mbili dhidi ya Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), najua hazitakuwa nyepesi lakini nina imani kwa jinsi tutakavyorekebisha kikosi chetu tunaweza kufanya vyema," alisema kocha huyo.

Amrouche amewakumbusha Watanzania timu yao ilikuwa inacheza na timu iliyofika hatua ya nusu fainali katika michuano iliyopita ya Kombe la Dunia.

„Kumbuka tumecheza na Timu ya Taifa ya Morocco iliyofika nusu fainali ya Kombe la Dunia lililopita, ni ngumu sana kushinda kutokana na aina na viwango vya wachezaji wao, lakini nadhani pia wachezaji wetu wamejifunza kucheza na wachezaji wakubwa wa aina ile, nafikiri pia kadi nyekundu iliyotolewa dakika ya 70 ilituathiri kwa sababu kabla ya hapo, tayari tulishaanza kuwasukumizia mashambulizi, lakini tutajipanga tu vizuri mechi zijazo," alisema kocha huyo raia wa Algeria na Ubelgiji.

Naye nyota wa Stars, Simon Msuva, aliwataka Watanzania waendelee kuwaunga mkono na anaamini makocha wameona mapungufu na wata-

INAENDELEA UK. 23



Adel Amrouche

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >